**JELA** miaka 30 kisa bangi Kg 38, eneo linaloongoza zakutwa ekari 100

UKURASA 5



**CCM** yaipa miezi 4 wizara kukamilisha uwanja wa ndege

UKURASA 19


BAJETI YA WIZARA YA NISHATI 2023/2024 — Nipashe 9

UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE

VYA BAJETI VYA MWAKA 2022/23 NA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2023/24

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Nishati

DODOMA
MEI, 2023

UKURASA 9


# Nipashe

Ijumaa Juni 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581329

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Dola zinavyouzwa kinyemela Kariakoo

UKURASA 2



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba

## Mkenda aonya shule binafsi kuzuia likizo kwa wanafunzi

UKURASA 2

## Mke aomba korti imtie hatiani mume mkopo benki

UKURASA 4

**MICHEZO** YANGA YAFUNGUKA HAPATOSHI ALGERIA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya REPOA, Dk. Donald Mmari (kushoto), akizungumza wakati wa mjadala kuhusu ongezeko la idadi ya watu na mabadiliko ya tabianchi, jijini Dar es Salaam juzi, ulioandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania kwa ushirikiano na Ubalozi wa Denmark nchini, katika maadhimisho ya wiki ya Nordic. Wengine ni Mia Mjengwa kutoka Taasisi ya Karibu Tanzania Organisation (kulia), Gerald Kihwele kutoka Wizara ya Afya (wa pili kulia) na Chiho Suzuki kutoka Benki ya Dunia. **PICHA: SABATO KASIKA.**

# Dola zinavyouzwa kinyemela Kariakoo

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya serikali na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kukemea ubadilishaji wa fedha za kigeni kufanyika kinyemela kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa nchini, biashara ya dola imeendelea kushamiri eneo la Kariakoo.

Uchunguzi wa Nipashe kwa miezi miwili eneo hilo, umebaini kuwa wafanyabiashara wa kigeni hubadilisha dola kwenye mitaa mbalimbali kisha kuziuza kwa kulangua au kuvizia zinapopanda bei.

Nipashe ilibaini limekuwa jambo la kawaida hasa kwa wafanyabiashara wanaoagiza mizigo nje ya nchi, kununua dola kwa wenzao kwa bei ya juu ili kupata pesa ya kumlipa wakala wa usafirishaji wa mizigo kwa lengo la kulipia mizigo hiyo katika nchi wanazoagiza.

Mfanyabishara wa nguo za kike Sinza, Vincent Michael, alisema kutokana na pesa hiyo kuadimika, baadhi ya wafanyabiashara wanatumia fursa hiyo kuwauzia dola kwa bei ya juu tofauti na bei elekezi. "Unakuta mfanyabiashara anahitaji Dola 20,000 akalipie mzigo kwa wakala, benki hawatoi zaidi ya Dola 2,000 kwa kila mteja kwa siku. Ili uipate yote hiyo itakulazimu uzunguke zaidi ya benki 10 au uende benki hiyo moja siku 10 lakini kuna mwenzako anazo na anataka rate (kiwango) yake," alisema.

Mfanyabiashara Martha Mrema alisema biashara hiyo imeshamiri kuanzia mwanzoni mwa mwaka huu na ndipo tatizo la upatikanaji wa dola lilipoanza. Kutokana na kununua Dola kwa bei ya juu, wanalazimika kupandisha bei ya bidhaa wanazouza ili kufidia gharama.

Christina Kaigo alisema wanapata pesa hizo kutoka kwa wageni wanaoingia kununua bidhaa za jumla. Alisema wageni hao ni kutoka Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambao huwauzia pesa ya Tanzania kwa gharama za chini tofauti na bei elekezi.

"Wateja wa kutoka mataifa ya nje mara nyingi wanakuja na dola na hawana muda wa kwenda benki kuchenji. Kwa hiyo wanakubaliana na kiwango kidogo wanachopewa. Kama dola inanunuliwa kwa Sh. 2,355 akija hapa tunanunua Sh. 2,255 na wanakubali. Wengine wanakuja na hata Dola 30,000," alisema.

Nipashe ilitembelea kwenye benki zikiwamo CRDB, I&M na NBC na kukuta Dola ya Kimarekani ikiuzwa kwa Sh. 2,410 hadi 2,415 kwa dola moja na kununuliwa kwa Sh.2,350.

Baadhi ya benki licha ya kuweka mabango kuonyesha bei ya kuuza na kununua Dola nje ya ofisi zao, zilikuwa haziuzi kwa madai kuwa hazina kwa muda huo.

Mmoja wa maofisa wa benki (jina linahifadhiwa) ambaye hakutaka kutajwa jina, alisema watu wanaouziwa Dola na fedha zingine za kigeni ni wateja wao tu na kiasi kisichozidi dola 2,000. Alisema kama mteja anataka zaidi ya hapo, atalazimika kuweka oda siku tatu kabla.

**BoT YAONYA**

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari juzi, Gavana wa BoT, Emanuel Tutuba, alipiga marufuku biashara ya fedha za kigeni na madalali wa kimataifa ambao hawajasajiliwa ndani ya Tanzania.

Aidha, aliwasihi madalali wa fedha za kigeni kuzingatia utaratibu wa kumtambua mteja kabla ya kufanya naye biashara na kuwa kiwango cha juu cha mizania kati ya mali na amana katika fedha za kigeni (NOP) kitakuwa asilimia 10 ya mtaji wa msingi na kinatakiwa kuzingatiwa muda wote.

**WATAALAM WASHAURI**

Meneja wa Fedha na Utawala wa Taasisi ya WAJIBU, CPA Jackson Mmari, alisema kuna haja ya kupunguza ununuzi wa vifaa kutoka nje ya nchi ili kuongeza mauzo ya bidhaa nchi hizo ili kuwa na pesa nyingi za kigeni zinazoingia kuliko zinazotoka.

"Kwa mfano tunavyojenga hizi reli, vifaa vingi vinanunuliwa nje ya nchi, malipo makubwa sana. Lakini pia kuna shughuli za kila siku kama vile kununua mafuta ambayo pia yanatumia dola," alisema.

Alishauri wawekezaji wajengewe mazingira rafiki kwa kufanya biashara ikiwamo uhakika wa pesa wanazozizalisha kwa sababu baadhi hutorosha kwa njia ya dola na kuziingiza kwenye benki za nchini kwao kwa kuhofia usalama wa wanachokizalisha.


## TAARIFA KWA UMMA



*Ms. Agnes Ndombela Sikwatta*

Sibusiso Foundation inapenda kutoa taarifa kwa wasambazaji, watoa huduma na umma kwa ujumla kwamba, Mkataba wa Meneja mkuu wetu Agnes Ndombela Sikwata ulimalizika tarehe **22 Mei 2023.** Kutokana na taarifa hii, Agnes Ndombela hatowakilisha tena Sibusiso Foundation kuanzia tarehe ya kuisha mkataba wake.

**Bodi ya Sibusiso Foundation**


# Mkenda azionya shule binafsi kuzuia likizo

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amezionya shule binafsi zinazozuia wanafunzi kwenda likizo bila kushauriana na wazazi huku zingine zikitaka wazazi walipe gharama za watoto hao kubaki shuleni.

Prof. Mkenda akitoa tamko la serikali kuhusu malalamiko ya wazazi ambao watoto wao wamebaki shuleni hususan wa madarasa ya mitihani, alisema jana kuwa ni vyema shule hizo zikazingatia waraka uliotolewa na Kamishna wa Elimu.

"Kwa shule binafsi kamishna alitoa unafuu kidogo kwamba waangalie ile kalenda, lakini wanaweza kufanya adjustment kulingana na mahitaji yao, ukweli unabakia palepale kwamba wanafunzi wetu wanahitaji kupumzika na mbaya zaidi kuna baadhi ya malalamiko tumeanza kupokea kwamba kuna shule zinazuia wanafunzi kwenda likizo bila hata kushauriana na wazazi na wengine wazazi wanatakiwa walipe kwa kuwaweka wanafunzi shuleni," alisema.

Alisema kwa shule za serikali kuna mwongozo umetolewa na Kamishna wa Elimu wa siku za kufunga shule na siku za kufungua ni muhimu wakajifunza kuzingatia mwongozo na wanafunzi kupata fursa ya kupumzika.

Alisema likizo zimewekwa kwa ajili ya wazazi wapate fursa ya kuwa watoto kucheza na kubadilisha mazingira inawasaidia na wataalamu wa elimu wanajua kuwa ni muhimu kufanya hivyo.

Waziri huyo alisema endapo malalamiko ya wazazi yataendelea, Kamishna wa Elimu atalazimika kutoa waraka.

**UTATA MIKOANI**

Bungeni jijini hapa jana, Mbunge wa Tarime Mjini, Michael Kembaki aliomba mwongozo wa Spika, akisema shule zinafungwa wiki hii na wizara imeagiza wadhibiti ubora kuzuia kambi zote za masomo katika kipindi cha likizo na baadhi ya mikoa imepanga utaratibu wa kuongeza ufaulu katika maeneo yao na wameagiza shule kuendelea na masomo ya ziada.

Baada ya maelezo hayo, Spika Tulia Ackson alimtaka Naibu Waziri wa Elimu kutoa ufafanuzi kuhusu mkanganyiko huo.

Naibu Waziri wa Elimu, Omary Kipanga, akitoa ufafanuzi bungeni, alisema hoja hiyo wameipokea na kwa mujibu wa sheria, wanafunzi wanatakiwa kusoma darasani siku 194 kwa mwaka.

Baada ya maelezo hayo, Spika alimtaka naibu waziri aeleze muda anaotaka kuja kutoa hayo maelezo, ndipo kiongozi huyo wa wizara alipoomba muda hadi kesho asubuhi atatoa ufafanuzi kuhusu mkanganyiko huo.

***Imeandaliwa na Augusta Njoji na Romana Mallya, DODOMA**

# Hoja ya January yapita wabunge wakitaka umeme kwa wananchi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WABUNGE wamepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati, wakitaka kuharakishwa usambazaji wa umeme na mradi wa kuunganisha gesi asilia majumbani.

Juzi Waziri wa Nishati, January Makamba alisema vijiji vyote nchini vitafikiwa na umeme kufikia mwezi Juni mwakani.

Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota (CCM), alisema ni vyema serikali ikaendelea kutenga fedha kwa ajili ya usambazaji wa nishati ya gesi asilia nyumbani.

Alisema takwimu zilizopo zinaonyesha Mkoa wa Mtwara tayari nyumba 420 zimeunganishiwa nishati hiyo na kwa Mkoa wa Lindi nyumba 209.

"Ninampongeza Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta ya nishati, lakini ninaomba fedha ziongezwe ili kasi iongezeke, ili wananchi wa Lindi na Mtwara wanufaike na gesi asilia na tupunguze matumizi ya kuni," alisema.

Chikota pia aliishauri serikali kuhakikisha inaishirikisha jamii katika utekelezaji wa mradi wa LNG. Aliitaja ni hatua itakayosaidia kuondoa migongano.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga, Mwanaisha Ulenge, alishauri Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere liwe kivutio cha watalii, ikizingatia kuwa limeungana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Mbunge wa Kibaha Mjini, Sylvester Koka, alimshukuru Rais Samia kwa kuruhusu maeneo ambayo yana mfumo wa REA kulipa Sh. 27,000 kuunganishwa umeme badala ya Sh. 320,000 hadi 350,000 zinazotozwa mjini.

Aliomba kupitia bajeti ya mwaka 2023/24, serikali ikahakikishe vijiji na wananchi wote waliorodheshwa wanaunganishiwa umeme kwa bei hiyo ya Sh. 27,000.

Mbunge wa Viti Maalum, Tauhida Cassian Gallos, alisema kushuka kwa gharama ya kununua umeme visiwani Zanzibar ni habari njema kwao, akisisitiza maneno yake hayo yanawakilisha wabunge wengine ambao pengine wasingepata nafasi ya kuzungumza.

"Tumepanga kwa makusudi wabunge wa Zanzibar kila atakayesimama tukupongeze kwa punguzo lililokwenda kushusha bei ya umeme Zanzibar. Mwaka jana kila mbunge wa Zanzibar aliyesimama, alikuwa analalamikia bei ya umeme inayokwenda Zanzibar. Ingawa jambo hili siyo la Muungano, waziri amekuwa msikivu na kutuliza kilio chetu," alisema.

Mbunge wa Newala Vijijini, Maimuna Mtanda, alisema kukatika umeme mkoani Mtwara limekuwa jambo la kawaida na umekuwa ukisababisha vifaa vya watu kuharibika na kuleta hofu kwa wananchi.

Pia alisema utekelezaji wa mradi wa REA mkoani humo uko sawa na mgonjwa aliye mahututi na kutaka wachukuliwe mkoa huo kama kesi maalum na isimamiwe.

# Eneo lililoongoza kwa bangi zakutwa ekari 101

**Na Waandishi Wetu**



SIKU chache baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenister Mhagama (pichani), kuwasilisha bungeni Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Mwaka 2022 nchini na kutaja maeneo yanayoongoza, ekari 101 za bangi zimeteketezwa katika eneo la Kisimiri Juu, Kata ya Uwalu, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

Eneo hilo lilitajwa katika taarifa hiyo na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kuwa linaongoza kwa kilimo cha bangi nchini. Ekari hizo zimeteketezwa huku kukiwa na mkakati wa kutafuta mazao mbadala kwa wananchi hao ili waachane na kilimo cha bangi.

DCEA imeteketeza ekari 101 za mashamba ya bangi sawa na kilogramu 550 za bangi mbichi pamoja na magunia 482 ya aina hiyo ya dawa za kulevya.

Jana, Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Aretas Lyimo, alisema uamuzi wa kuteketeza dawa hizo unatokana na maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kutaka kufanyika utafiti kujua ni mazao gani mbadala yanaweza kulimwa katika maeneo hayo.

"Rais Samia ameamua ufanyike utafiti katika maeneo hayo, ambayo yamekithiri kwa kilimo cha dawa za kulevya ili wananchi wa maeneo husika wapewe mbinu mbadala za kulima mazao mbalimbali ya chakula na biashara, badala ya kuendelea na kilimo cha bangi.

"Aidha, ukamataji huo na kisha uteketezaji umefanyika kutokana na agizo la Rais la kutaka kufanyika operesheni nchi nzima, ili kuhakikisha dawa za kulevya zinatokomezwa," alisema.

Kuhusu operesheni za kushtukiza, Kamishna Jenerali Lyimo, alisema mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, itaendelea kufanya operesheni za mara kwa mara katika maeneo hayo, ili kuhakikisha bangi inatokomea kabisa mkoani humo.

"Tumewasiliana na Wizara ya Kilimo na Ofisa Kilimo wa Kata ya Uwalu-Kisimiri na amenieleza tayari utafiti huo umefanyika," alisisitiza.

Kamishna Lyimo alisema elimu juu ya athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevya, itatolewa kupitia shule za msingi na sekondari.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu utafiti huo, Ofisa Kilimo wa Kata ya Uwelu, Samwel Palangyo, alisema utafiti uliofanywa na Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Tenguru, umebaini kuwa yapo mazao yanayostawi katika maeneo hayo kama pareto, karoti na viazi mviringo.

Palangyo alisema kutokana na utafiti kukamilika, anaiomba serikali kuangalia namna ya kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kwa kutoa ruzuku ya mazao hayo.

Wakati hayo yakiendelea Arusha, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kibaha imemtia hatiani na kumuhukumu kifungo cha miaka 30 jela Abubakar Mbanje kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi kilo 38.84.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Hakimu Mkazi Salumu Ally baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Baada ya kutiwa hatiani mshtakiwa aliomba mahakama imwonee huruma, ana familia inamtegemea, akaomba aachiwe huru, lakini Hakimu Salumu alisema kuwa licha ya kuzingatia maombi ya mshtakiwa, kutokana na ukubwa wa kosa hilo mahakama inampa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

Awali ilidaiwa mahakamani kuwa mtuhumiwa alikamatwa na DCEA Mei 19, 2022 katika eneo la bandari bubu iliyopo Mlingotini - mji mpya, Wilaya ya Bagamoyo akiwa na kilo 38.84 za dawa ya kulevya aina ya bangi alizokuwa akizisafirisha kwa kutumia pikipiki.


TAARIFA KWA UMMA

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

KUANZISHWA KWA OFISI MPYA YA NSSF UBUNGO NA KUHAMA KWA OFISI YA NSSF KINONDONI

**Dar es Salaam, 01 Juni 2023**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unapenda kuwataarifu Wanachama, Waajiri na Umma kwa ujumla kuhusu kuanzishwa kwa Ofisi mpya ya NSSF Ubungo katika jengo la Ubungo Plaza. Ofisi hii imeanza rasmi kutoa huduma tarehe 1 Juni, 2023.

Aidha, Ofisi ya NSSF Kinondoni iliyokuwa kwenye jengo la Ubungo Plaza imehamishiwa kwenye jengo la Millenium Tower lililopo eneo la Makumbusho - Kijitonyama. Ofisi hii imeanza rasmi kutoa huduma tarehe 1 Juni, 2023.

Lengo la kuanzishwa kwa ofisi mpya ya Ubungo na kuhamishwa kwa ofisi ya Kinondoni ni kusogeza huduma zitolewazo na Mfuko karibu zaidi na wateja.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia simu ya bure 0800116773 au tembelea ofisi ya NSSF iliyo karibu nawe.

Imetolewa na: **Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma**

Simu Bure 0800116773

NSSF

@NssfTanzania




Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Nasoro Ngoma (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa kwenye Maonyesho ya Madini mjini Lindi hivi karibuni. Kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Wachimba madini wanawake nchini, Palina Ninja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# CRDB yageukia kuwawezesha wanawake wachimba madini

**Na Mwandishi Wetu,** RUANGWA

IKIWA imeshakopesha zaidi ya bilioni 67 katika sekta ya madini katika robo ya kwanza ya mwaka huu, Benki ya CRDB imewakaribisha wanawake wachimba madini kunufaika na fursa ilizonazo hasa kupitia programu yake ya Imbeju.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa, alitoa hamasa hiyo jana katika maonyesho ya madini yaliyofanyika mkoani Lindi na kuwahusisha wanawake waliojishughulisha na sekta hiyo nchini.

"Benki ya CRDB ni mdau mkubwa wa sekta ya madini nchini. Kuanzia Januari mpaka Machi mwaka huu tumekopesha zaidi ya Sh. bilioni 67 katika sekta ya madini pekee.

"Ninakipongeza Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini Tanzania (TAWOMA) kwa kuandaa tamasha hili linalolenga kuibua fursa kwa wanawake katika mikoa ya kusini hasa mkoani Lindi. Jitihada hizi zitahamasisha ushiriki wa wananchi katika uchimbaji wa madini ya kimkakati nchini hasa madini ya kinywe (graphite) yanayopatikana hapa Ruangwa. Kweli kusini kuchere," alisema Tully.

Mwanzoni mwa mwaka jana, Benki ya CRDB iliingia makubaliano na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini kupata mikopo itakayoimarisha shughuli zao. Katika robo ya kwanza mwaka huu, Tully ambaye ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB alisema wamekopesha zaidi ya Sh, bilioni sita kwa kundi hilo.

Sio kwa madini pekee, Benki ya CRDB ni taasisi inayolipa uzito suala la uwezeshaji wanawake, hivyo kulitambua kundi hilo kama lenye uhitaji maalum. Kwa kuyatambua mahitaji maalum ya wanawake, benki imeanzisha Taasisi ya CRDB Bank Foundation iliyojikita kusimamia programu endelevu za kuwawezesha wanawake na vijana nchini.

"Hadi Mei 26, Taasisi yetu ya CRDB Bank Foundation ilikuwa imewafikia jumla ya wanawake 10,238 na kuwapa elimu kabla ya kuwapa mtaji wezeshi wa kukuza biashara zao.

"Mafunzo hayo ya Imbeju yalifanyika pia katika kongamano hilo la madini yakiambatana na elimu ya bima, uendeshaji biashara, utafutaji masoko, kodi, urasimishaji biashara na mambo mengine muhimu.

"Jitihada hizi za kuwafikia wanawake zinaendelea katika mikoa mbalimbali nchini na ninafurahi kupitia Lindi Madini Festival tumepata nafasi ya kuendelea kuifikisha hapa ili kuwawezesha wanawake wa mkoa huu kujikwamua kiuchumi na kuchochea maendeleo ya Mkoa wa Lindi na taifa kwa ujumla," alisema Tully.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake Wachimba Madini Tanzania, Palina Ninja, alisema iwapo benki zitawapa nafasi ya kupata mikopo ya kukuza shughuli zao, uchumi wa familia nyingi nchini utaimarika, hivyo kurahisisha vita dhidi ya umaskini.

"Mama akiwa na kipato cha uhakika, uchumi wa familia utakua. Tunaziomba benki za biashara nchini kutulegezea masharti ili tukopesheke kwa urahisi. Uaminifu wa mwanamke katika kurudisha mkopo unafahamika. Sekta ya madini ina fursa kubwa ya kupunguza umaskini iwapo wanawake wengi watashiriki," alisema Palina.

Mgeni rasmi katika maonyesho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, alisema serikali inaendelea kuondoa vikwazo vya kufanya biashara nchini ili kila mjasiriamali anufaike na fursa anazoziona mbele yake.

Ili kurahisisha upatikanaji wa mitaji, Ngoma alisema serikali itaendelea kutunga sera rafiki kama ilivyofanya katika kilimo ambako imetenga mikopo kwa taasisi za fedha zitakazokopesha kwa chini ya asilimia 10 ili kuwezesha uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara.

# Mke aomba mumewe atiwe hatiani kutaka kuuza nyumba

**Na Kulwa Mzee**

MKE wa Selemani Maziku, Skola Godfrey, ameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu imtie hatiani mumewe kwa kutaka kuuza nyumba ya familia baada ya kishindwa kurejesha mkopo wa benki.

Skola aliwasilisha ombi hilo jana katika mahakama hiyo alipotoa ushahidi dhidi ya mumewe anayekabiliwa na mashtaka ya kughushi saini ya mke wake (Skola) na kisha kwenda kuchukua mkopo benki bila kumtaarifu.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Erick Kamala, Skola alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio kuwa mwaka 2014, maofisa wa Benki ya Stanbick walifika nyumbani kwao eneo la Kitunda Mwanagati na kupiga mnada nyumba yao.

Alidai benki ilifikia uamuzi huo kwa kuwa mumewe Maziku alichukua mkopo unaodaiwa kuwa Sh. milioni 140 na kushindwa kuurejesha.

Skola alidai kuwa maofisa hao wa benki hawakufanikiwa kuuza nyumba hiyo kutokana na kukosa mteja.

Alidai kuwa mumewe Selemani alimwambia atafanya mpango wa kurejesha fedha hizo, lakini hakumshirikisha katika hatua yoyote ya uchukuaji mkopo huo.

"Maisha yaliendela na ilipofika mwaka 2020, nilifanikiwa kuona nyaraka za maombi ya mkopo huo ambazo ziliosnyesha jina, picha yake na saini ambayo haikuwa yangu.

"Katika nyaraka hizo kulikuwa na nyaraka ambayo ilinitambulisha mimi kama mpangaji katika nyumba yetu hiyo ambayo pia ilionyesha imetiwa saini na mtu mwingine.

"Nilishtuka kuona mimi ni mpangaji katika nyumba yetu, saini iliyo katika nyaraka ya maombi ya mkopo benki sio yangu kwa sababu sijawahi kutia saini nyaraka zozote benki ama mbele ya mwanasheria," alidai.

Shahidi huyo alidai aliumia sana. Akaamua kuondoka nyumbani. Hivyo, akaiomba mahakama imtie hatiani mumewe kwa kughushi saini yake na kutaka kuuza nyumba ya familia.

Akijibu hoja za upande wa utetezi, Skola alidai hakuwahi kushuhudia nyaraka za mkopo huo ulivyokuwa umeandaliwa.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Juni 27 mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Katika shauri hilo, inadaiwa kwamba Desemba 10, 2022, katika eneo lisilofahamika mkoani Dar es Salaam, mshtakiwa, bila ridhaa kutoka kwa mkewe Skola Godfrey, alitia saini ridhaa ya mwenza katika mkopo akionyesha imetiwa saini na Skola.

# Ma-DED watakiwa kuzingatia uwiano watumishi afya kwenye maeneo yao

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SERIKALI imetoa maelekeo kwa wakurugenzi kufanya mapitio ya kina kwa baadhi ya watumishi wa afya walionao na maeneo yenye mrundikano mkubwa kuwahamisha na kuwapeleka kwenye upungufu huo.

Majaliwa aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akijibu maswali ya papo kwa hapo ya wabunge.

Mbunge wa Jimbo la Mvumi, Livingstone Lusinde, alisema serikali imefanya kazi kubwa ya ujenzi wa vituo vya afya sambamba na kazi hiyo vile vile imepeleka vifaa tiba karibu kwenye vituo vyote vya afya.

Hata hivyo, kumekuwa na upungufu mkubwa wa wataalam katika vituo hivyo wa kutumia mashine na vifaa tiba vilivyopelekwa na serikali na kutaka kujua, serikali ina mpango gani wa kuwapeleka wataalam huko ili vifaa viweze kutumika na kuokoa maisha ya Watanzania.

Katika majibu ya swali hilo, Majaliwa alisema, "Ninaungana naye, serikali yetu toka Awamu ya Tano mpaka Awamu ya Sita, imefanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa maeneo ya kutolea huduma nchini zahanati, vituo vya afya, hospitali za halmashauri za wilaya.

"Lakini pia, mikoa na kanda na sasa tunaimarisha huduma kwenye hospitali za kitaifa, ninampongeza rais kwa maelekezo yake na kwa usimamizi wake na sisi tunaendelea kuimarisha maeneo haya ya utoaji huduma.

"Awamu ya kwanza ilikuwa ni kujenga miundombinu na majengo kazi hiyo imefanywa vizuri nataka niwahakikishie Watanzania tutaendelea kujenga vituo vya afya na zahanati kulingana na mahitaji kwenye halmashauri na vijiji," alisema.

Majaliwa alisema awamu ya pili ni ya kupeleka vifaa tiba na dawa kazi ambayo kwa sasa inaendelea kwa kasi. Baada ya majengo tunaweka vifaa vya maabara, lakini pia, dawa na vifaa vingine, vitanda kwenye wodi, kazi hii pia inaendelea vizuri," alisema.

Alisema mpango wa serikali wa kupeleka watumishi, kazi hiyo inaendelea vizuri na kwamba, Rais Samia ameshatoa vibali kwa Wizara ya Afya pamoja na mamlaka za serikali za mitaa kuajiri watumishi wa sekta ya afya ili kuwapeleka kwenye maeneo hayo yote kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali zote ili waweze kutoa huduma.

Alisema wanajua wana maeneo mengi ya kutolea huduma ambayo mahitaji ni makubwa kulinganisha na ikama kwa hiyo serikali itaendelea kuajiri kutokana na uwezo wa kifedha kwa lengo la kutoa huduma kwa Watanzania kwenye maeneo yao.

"Wakati huo tulipewa kibali, lakini pia huku ndani tunafanya mapitio kwa sababu tunajua kuwa maeneo mengine yana watumishi wengi zaidi kuliko mengine kwa hiyo tunahamisha walikojaa kupeleka ambako hakuna watumishi hasa kutoka mjini ambako kuna mrundikano kwenda vijijini ili maeneo yote yaweze kupata huduma. Pia alisema, wale walioko wanawajengea uwezo kwa kuwapeleka kwenye mafunzo ili waweze kutoa huduma kwa urahisi zaidi.

"Nitoe pia maelekezo kwa wakurugenzi wafanye mapitio ya kina ya idadi ya watumishi tulio nao na maeneo yenye mrundikano mkubwa kuwahamisha na kuwapeleka kwenye maeneo yenye watumishi wachache ili huduma zitolewe kwa usawa kwenye maeneo yote.

# Majaliwa aagiza Ma-DC kuzuia kero michango holela shuleni

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani), amewaagiza wakuu wa wilaya nchini kuhakikisha hakuna michango holela shuleni inayokera wananchi na kushindwa kufanya shughuli nyingine huku wanafunzi nao wakiondolewa shuleni.

Pia amewataka wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha wanatoa huduma hizo shuleni na kuweka mpango mzuri katika maeneo yenye uhitaji.

Majaliwa alielekeza hayo jana bungeni jijini hapa alipojibu maswali ya wabunge wakati wa kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu'.

Mbunge wa Kilwa Kusini, Ali Kasinge, alisema serikali imekuwa inatekeleza sera yake ya kutoa elimumsingi bila malipo, maarufu elimu bure, kwa lengo la kuwapunguzia gharama wazazi na walezi.

Lakini, kumekuwa na michango kadhaa katika shule za umma ikiwamo michango ya ulinzi, shajara (diary) na chakula, akihoji serikali haioni umuhimu wa kupitia sera hiyo ili michango hiyo inayobebwa na wazazi na walezi iwe ni jukumu la serikali kwa dhana ileile ya kuwapunguzia gharama wazazi na walezi.

Majaliwa, akijibu swali hilo, alisema serikali inaendelea kutekeleza sera hiyo kwa lengo la kuwaondolea wazazi adha ya michango mingi na ile holela.

"Kila mwezi serikali hupeleka fedha katika halmashauri kwa ajili ya kuwezesha shule za sekondari, wale wakuu wa shule huzitumia katika maeneo ambayo walitegemea kupata michango kutoka kwa wazazi ili wasichangie badala yake wazazi waendelee kusimamia maboresho ya mtoto kwenda shuleni ikiwamo kununua sare na mengineyo," alisema.

Waziri Mkuu alisema anatambua kwamba si maeneo yote yameweza kupata fedha, hasa eneo la chakula na ulinzi.

"Maeneo tuliyotolea fedha ni yale ya ukarabati wa majengo mdogo, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vitabu, chaki na vingine ili kuondoa adha ya walimu kuchangisha wazazi," alisema.

Majaliwa alisema eneo ambao sasa wanaendelea kushughulika nalo ni maboresho. Alisema zipo shule nyingi za sekondari ambazo wanafunzi wanakwenda asubuhi na kurejea jioni na wanapokuwa shuleni hawapati chakula.

"Eneo hili nikiri kwamba serikali tunaendelea kuchakata ili kuona namna nzuri ya kutoa huduma ya chakula shuleni ingawa tumeona sekta binafsi zinashiriki, wakati mwingine wazazi wenyewe wanaweka mpango wao.

"Niliposema michango holela ni ile ambayo walimu wanasema njoo kesho na Sh. 200, Sh. 1,000, Sh. 500 ambazo zinakera wazazi, hiyo tumeidhibiti na tumepiga marufuku na haipo kabisa.

"Na kama iko tulishatoa maelekezo hapa pia, nitatoa maelekezo, sisi tunaruhusu michango rasmi inayokwenda kufanya shughuli za maendeleo.

"Shule za msingi na za sekondari hizi ni shule za wananchi. Kila kijiji kina shule za msingi, zinasimamiwa na kijiji chenyewe. Inapotokea choo kimebomoka hatuzuii wazazi kukaa na kujenga kwa kuchangishana, hii ni michango ya maendeleo, ingawa michango hii tumeiwekea



masharti kidogo, anayetakiwa kusimamia michango ni mkuu wa wilaya pekee au yeyote ambaye kiongozi huyu amemchagua kusimamia. Tunaogopa watu kuchangisha kiholela," alisema.

Waziri Mkuu alisma serikali inaendelea kufanya mapitio ya sera ili kuwezesha mzazi kupata unafuu zaidi wa kutoa michango kwa ajili ya maboresho ya shule.

Pia alisema bado hawaondoi nafasi ya uwajibikaji wa wananchi shuleni katika kufanya maboresho.

"Niliposema mkuu wa wilaya mstaafu (mbunge aliyeuliza swali) ninajua hili ulilisimamia vizuri sana ulipokuwa mkuu wa wilaya kabla hujawa mbunge. Serikali itaendelea kusimamia haya.

"Nitoe wito pia kwa halmashauri isimamie kupitia bajeti zao kama ni lazima kuzungumza na wazazi.

Lakini pia wazazi kuzungumza na kamati zao za uamuzi, haya ndiyo tunayasimamia kwa sasa. Ombi la mheshimiwa mbunge la kufanya maboresho ya sera yetu tumeyapokea na tutayafanyia kazi," alisema.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanafunzi waachwe wapumzike wakati wa likizo

**SERIKALI** kupitia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, imezionya shule binafsi zinazozuia wanafunzi kwenda likizo.

Hatua hiyo ya serikali inatokana na baadhi ya shule binafsi kuwazuia wanafunzi kwenda likizo nyumbani na kubaki shuleni, huku wakiendelea kuwatoza gharama za kubaki shule wazazi wa wanafunzi hao.

Baadhi ya shule hizo zimebainika kuwa zinachukua uamuazi huo bila kushauriana na wazazi wa wanafunzi hao, kitendo ambacho hakikubaliki.

Hali hii inaweza kusababisha mtoto akasingizia kutakiwa kubaki shuleni na kwenda kufanya mambo ya ovyo, huku mzazi akijua kuwa mtoto wake yuko shuleni.

Zuio hilo linatokana na malalamiko ya wazazi ambao watoto wao wamebaki shule hususan wa madarasa ya mitihani.

Serikali imezionya shule hizo na kuzitaka kuzingatia waraka uliotolewa na Kamishna wa Elimu.

"Kwa shule binafsi Kamishna alitoa unafuu kidogo kwamba waangalie ile kalenda, lakini wanaweza kufanya adjustment kulingana na mahitaji yao, ukweli unabakia palepale kwamba wanafunzi wetu wanahitaji kupumzika na baya zaidi kuna baadhi ya malalamiko tumeanza kupokea kwamba kuna shule zinazuia wanafunzi kwenda likizo bila hata kushauriana na wazazi na wengine wazazi wanatakiwa walipe kwa kuwaweka wanafunzi shuleni."

Kwa shule za serikali kuna mwongozo umetolewa na Kamishna wa Elimu wa siku za kufunga shule na siku za kufungua ambao ni muhimu shule binafsi zikajifunza kuzingatia mwongozo na wanafunzi kupata fursa ya kupumzika.

Wakuu wa shule wote na wakurugenzi wametakiwa kuzingatia utaratibu huo na wito wa serikali ni kwamba shule hizo zisimlazimishe kamishna atoe waraka wenye masharti makali kwa sekta binafsi.

Wamiliki wa shule lazima wazingatie kuwa likizo zimewekwa kwa ajili ya wazazi kupata fursa ya kuwa na watoto wao kucheza na kubadilisha mazingira ambayo inawasaidia na wataalamu wa elimu wanajua kuwa ni muhimu kufanya hivyo.

Umuhimu wa likizo pia unamsaidia mzazi kuzungumza na mtoto wake, kujua changamoto zinazomkabili, maadili yake na vile vile kujua maendeleo yake kimasomo. Mtoto anapozuiwa kubaki shule, matokeo yake ni kumfanya mzazi na mtoto mwenyewe kushindwa kupeana taarifa.

Ndiyo maana baadhi ya watoto wanapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia wanashindwa kuwaeleza wazazi wao kwa sababu ya kukosa ukaribu wao.

Tamko hilo la serikali linazihimiza shule zizingatie agizo hilo na pale ambapo kuna makubaliano na wazazi kwa shule binafsi kwamba watoto wakae yawe makubaliano ya hiyari sio ya kulazimishana na pamoja na kuongeza muda kidogo kama wameamua kuongeza kwa ajili ya maandalizi, lakini lazima watoe muda kwa watoto, vilevile kwenda kupumzika.

Hata hivyo, Waziri anayehusika na elimu ameonya kuwa endapo malalamiko ya wazazi yataendelea, Kamishna wa Elimu atalazimika kutoa waraka. Cha msingi ni shule kuzingatia agizo lililotolewa ili zisilazimishe serikali kuchukua hatua kali na baadaye kuziathiri shule nyingine.

Mtoto lazima apewe haki yake ya kupumzika, anapohenyeshwa inaweza pia kumuathiri katika masomo na badala ya kumsaidia, ikamharibia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Karibu sana RC Makalla, sisi wana Mwanza machache yetu haya hapa

Na Anthony Gervas, Mwanza.

**TUNAKUKARIBISHA** mgeni, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, ukitokea Dar-es Salaam, ambaye tunaamini sasa umekuja hapa mkoani tuungane pamoja kuchapa kazi za maendeleo na wananchi ukiwa umeshikilia makali ya kaulimbinu "Kazi Iendelee'

Naam! Wewe sasa ni jemedari wetu, tunakutegemea utuvushe pale tulipo kwenda sehemu nyingine kimaendeleo, kiuchumi, biashara na mengine,tuko nyuma yako tukifuata nyayo.

Mkoa wa Mwanza una fursa nyingi hujawahi kuona,mfano kuna madini ya dhahabu,uvuvi wa samaki Ziwa Victoria, tuna ardhi yenye rutuba ya kutosha kwa kila aina ya kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

Mfano ni kilimo cha pamba, mahindi, njugumawe, alizeti, choroko, kunde, mtama, viazi vitamu, nyanya, miwa, dengu, mpunga, mihogo na mengine mengi. Tatizo kubwa linalozorotesha shughuli za maendeleo na uzalishaji, ni usimamizi duni wa baadhi ya watendaji wetu, ambao wanasubiri mpaka wasukumwe.

Kuna haja ya watendaji kubadilika tabia, wajitume bila kusukumwa, kwa sababu kila mtu anatakiwa kuipenda kazi aliyoichagua,siyo ubabaishaji wakati wanalipwa mishahara itokanayo na kodi za wananchi. Kama ulichagua kazi hiyo, inapaswa uitendee haki.

Kwa ujumla, ni mkoa wa wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara, wafugaji, wavuvi, viwanda mbalimbali vilivyosheheni rasilimali za kutosha, zikiwamo vivutio vya visiwa, Hifadhi ya Taifa ya Saanane, iliyoko ndani ya Ziwa Victoria, milima na shughuli za uwekezaji.

Hakuna shaka wananchi wanaamini sasa fursa hizo zitawanufaisha zaidi, kwa usimamizi wako uliotukuka,wewe ni dhamana kwa kuwa serikali imekuamini, kwamba uje hapa kuwatumikia wananchi, ikiwamo kusikiliza shida za masikini. Tunaamini ofisi yako itakuwa wazi kwa ajili ya kuwahudumia wana Mwanza wote bila ubaguzi wa matabaka.

Mwanza imesheheni utajiri. Wapo watu wengine huenda wanaitamani kuwa ingekuwa kwao, sasa msamiati wa 'mgeni njoo wenyeji tupone'unao ofisini kwako, tofauti na hapo itabadilika kuwa 'mgeni njoo wenyeji tuumie.' Tunajua ndiyo umeanza kufanya kazi mwishoni mwa mwezi ulioisha juzi.

Hili ni jiji maarufu Tanzania katika ukanda wa Kanda ya Ziwa na Afrika Mashariki kwa ujumla. Wengi wanatamani waje kujionea fursa zilizopo, kujua historia yake ya utalii uliopo ndani na mandhari zinazovutia kila kukicha.

Makalla wewe ndiye umeshika makali, ukitangulia vitani kupambana na majukumu,kero za mkoa zote ni zako. Mafanikio ya vyote vitakupa sifa, yetu ni macho na masikio tunakusubiri utekelezaji wako ututangulie na usituangushe kwa dhamana kubwa uliyopewa.

Zipo changamoto zinazowaumiza wananchi, ambazo zinatakiwa kusimamiwa,mfano ujenzi miradi ya barabara, masoko, kudhibiti ufujaji fedha za umma kwenye miradi, ambayo kimsingi ni kero kubwa kwa wananchi.

Yawezekana, mkuu wetu ukawa umekuja na mpango mkakati kabambe ambao utaibadilisha Mwanza kiuchumi, ikiwamo usafi wa mazingira, kumaliza kero ya machinga katika kuboresha masoko yao wanakofanyia biashara.

Tufahamu kila mahali hapakosi changamoto, misukosuko, migongano, lakini wewe kiongozi wetu umejaa hekima na busara, tunaamini utatuvusha tulipo, hatuna shaka wananchi wataungana nawe kusukuma zigo la maendeleo.

Pia, tunakukumbusha wana Mwanza kuwa kwenye ofisi yako usisahau kuwahamisha watumishi waliokaa muda mrefu bila kuhama, wengine wakiwa na zaidi ya miaka 10, ambao wameshajenga mazoea ya kimaslahi yao binafsi.

Wananchi hawahitaji mpaka wawanyoshee vidole kwamba watumishi hao wamewachoka, wanahitaji kubadilishwa vituo vya kazi, ili kama wamezoea kwenda kinyume na maadili ya kazi, ukiwamo 'upigaji' waende huko kwingine wakaumbuke, hata Waswahili wananena mazoea hujenga tabia.

Unafahamu binadamu hapendi kuambiwa ukweli. Katika hilo tunaikosoa serikali kuacha watumishi wa umma wakikaa miaka mingi wakilinda maslahi yao binafsi au maslahi ya nani? Wanawaumiza wananchi wengi ,kwanini hawahamishwi? Au wako pale mahsusi kwa ajili ya watu flani kulinda maslahi yao.

Makalla, jambo hilo limekuwa likilalamikiwa na wananchi hivyo hao waliokaa miaka mingi wachunguzwe kuna nini nyuma ya pazia?.

# UNDP yatangaza neema kwa wajasiriamali nchini

**Na Maulid Mmbaga**

WAJASIRIAMALI wa ubunifu nchini wanaendelea kunufaika na uwekezaji wa Sh. bilioni nne iliyotolewa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU) baada ya kuzinduliwa kwa awamu ya pili ya ufadhili yenye lengo la kuwawezesha kuichumi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi wakati wa hafla ya uzinduzi wa awamu ya pili ya ufadhili kwa wajasiriamali nchini uliofanyia juzi jijini Dar as Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Erasto Mluyka, alisema serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wadau mbalimbali wanaojitolea kusaidia bunifu nchini.

Alisema tume hiyo inaibua wabunifu kutoka ngazi ya chini na kuwaandaa vijana mbalimbali wabunifu ili waweze kufikiwa na wadau wengine wanaohusika na ufadhili wa masuala ya ubunifu kama Programu ya FUNGUO.

"Programu hiyo ili iweze kusaidia hao wabunifu, inahitaji kuona tayari ameshaanza kufanya biashara ya kibunifu, hivyo, ili waweze kufikiwa serikali inawekeza kiwango cha kuanzia Sh. milioni moja hadi 30, kwenye kuwaandaa wabunifu kupitia Dar Teknohama Business Incubator (DTBi)," alisema na kuongeza:

"FUNGUO imewekeza kuanzia kiwango cha Sh. milioni 50 hadi 100 kwa mbunifu, hivyo imesaidia jitihada za serikali ambazo imezianzisha na kwa kushirikiana nao tutaenda kutengeneza ajira nyingi kwa vijana na kuwezesha uchumi wa nchi na kuifanya nchi iwe shindani katika masuala ya teknolojia na uchumi," alisema Mluyka. Mwakilishi mkazi wa UNDP nchini, Christine Musisi, alisema kutokana na kuwapo kwa idadi kubwa ya vijana nchini inawapa fursa kubwa ya kuwekeza kwao na kuwawezesha kuunda hatima yao wenyewe kwa kutumia nguvu, welevu na ubunifu. Alisema kuzinduliwa kwa awamu ya pili ya maombi ya ufadhili chini ya FUNGUO kunaashiria hatua nyingine muhimu katika kujitolea kwa UNDP kukuza uvumbuzi na kuendesha malengo ya maendeleo ya kitaifa.

"Tunaamini kabisa uwezo wa vijana wengi wabunifu wanaojitolea kuleta mabadiliko chanya kupitia ujasiriamali, juhudi zao sio tu kuwatengenezea fursa za ajira na vijana wenzao bali pia zinachangia maendeleo endelevu ya taifa letu.

"UNDP inasalia kujitolea kuwasaidia kupitia mipango kama vile FUNGUO, shukrani kwa uungwaji mkono usioyumba wa washirika wetu, kama vile Umoja wa Ulaya na Serikali ya Uingereza," alisema Christine. Mkuu wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Cedric Merel, alieleza kuwa kwa EU ni muhimu kuunga mkono ukuaji na ubunifu wa sekta binafsi kama wanavyotoa msaada kwa serikali kuongeza mifumo na mchakato wa kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.




Mwanzilishi wa Jukwaa la Niajiri, Lilian Madeje (katikati), akichangia mada katika mdahalo kuhusu programu ya uwezeshaji wa wananchi kuimarisha uwezo wa vijana kuajirika pamoja na kuendesha biashara kupitia mikopo ulioandaliwa na Taasisi ya Aga Khan Foundation, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja Miradi wa Taasisi hiyo, Simon Migaro na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoani Mtwara, Juliana Manyama. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# UWATANGUTA yaiangukia serikali makato ya asilimia 10

**Na Jenifer Gilla**

UMOJA wa Makandarasi wa Taka Ngumu Tanzania (UWATANGUTA), umeiomba serikali kupunguza makato ya asilimia 10 wanayokatwa na halmashauri kabla ya kutoa gharama za uendeshaji kwa kuwa inarudisha nyuma utendaji kazi wao.

Pia wameiomba kuboreshwa mikataba wanayoingia kufanya nao kazi kutoka mwaka mmoja na miwili hadi angalau miaka mitano ili wapate fursa nzuri za kiuchumi ikiwamo mikopo ya benki.

Mwenyekiti wa umoja huo kitaifa, Mary Ramadhani, aliiambia Nipashe kuwa kitendo cha manispaa kukata asilimia 10 ya makusanyo ya kodi kabla ya mkandarasi kutoa gharama za uendeshaji wa shughuli hizo kinarudisha nyuma utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwa pesa nyingi inakwenda serikalini.

Kutokana na hali hiyo aliiomba serikali ikate makato hayo baada ya mkandarasi kutoa gharama za uendeshaji ili wapate pesa za kufanyia marekebisho na maboresho ya vitendea kazi vyao.

"Haiwezekani vifaa vyote vya kazi nitoe mimi (mkandarasi) halafu serikali ichukue hadi pesa za gharama za uendeshaji, tunashindwa kufanya matengenezo ya uhakika kwenye magari yetu matokeo yake yanazidi kuwa mabovu, magari yanaweza kukaa hata wiki mbili hayafanyi kazi kwa kuwa yameharibika na hatuna pesa ya kufanya marekebisho," alisema.

Aidha, alisema kuna umuhimu mikataba wanayopewa iwe na masharti mepesi ili wawe huru kufanya kazi zao na wapate muda wa kusoma mazingira wanayotakiwa kusimamia kwa usafi.

Mweka hazina umoja huo kitaifa, Ntuli Damson, alisema baadhi ya mikataba wanayoingia na halmashauri mbalimbali ni mifupi, inawanyima fursa ya kukopesheka benki kwa kuwa haiendani na muda wa marejesho.

"Mikataba inasababisha tunashindwa kufanya uwekezaji kwenye teknolojia za kisasa kama kununua magari ya kisasa ya kuzoa taka na hivyo hulazimika kutumia magari chakavu au mabovu," alisema.

Alitaja changamoto nyingine ni ucheleweshaji wa malipo kutoka katika halmashauri hali inayowafanya kushindwa kulipa kodi kama za Mamlaka ya Mapato (TRA), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kulipa mishahara ya wafanyakazi kwa wakati.

"Unavyotuona hapa tuna madeni makubwa TRA, NSSF, wafanyakazi wetu wanafanya kazi kwa weledi na uvumilivu mkubwa, lakini tunachelewa kuwapa mishahara, ninaamini kodi ya asilimia 10 ikiboreshwa haya yote yatakwisha," alisema.

Mmoja wa mkandarasi wa taka ngumu aliyekuwa akikusanya taka Manispaa ya Temeke na Ilala, Dary Makwama, alisema aliamua kuacha biashara hiyo baada ya kutofanya vizuri kutokana na madeni anayozidai manispaa hizo tangu mwaka 2012.

"Niliamua kuacha baada ya kuona biashara haiendi vizuri, madeni yanazidi kuongezeka wakati pesa zangu manispaa hawanilipi. Ninaidai Manispaa ya Ilala Shilingi bilioni mbili na Temeke milioni 400 baada ya kuwakodisha magari yangu wazolee taka, hawajanilipa mpaka leo wakati nilichukua mkopo benki," alisema.

# Ndege ya mizigo kutua Dar kesho

**Na Joseph Mwendapole**

NDEGE kubwa ya mizigo aina ya Boeing 767 inatarajiwa kuwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) kesho na Tanzania kuweka historia kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa na ndege hiyo.

Ndege hiyo itapokewa na Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi mbalimbali ikitokea moja kwa moja Marekani.

Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, alilithibitishia gazeti hili juzi kuwa taratibu zote za ndege hiyo kuwasili Jumamosi zimekamilika na hafla ya ujio wake itaonyeshwa moja kwa moja na vyombo vingi vya habari.

"Ni kweli ndege itawasili tarehe 3 Juni ambayo ni Jumamosi na mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ndiye atakayeipokea pamoja na viongozi mbalimbali," alisema Msigwa.

Aidha, aliwataka Watanzania wapuuze taarifa zilizotolewa kwenye mtandao mmoja kwamba ndege hiyo imebeba mizigo ambayo haijalipiwa kodi kwa nia ya kuchafua nchi.

"Ninaomba Watanzania wakiona hicho kitu wawapuuze hawa watu kwasababu ndege yenyewe ndiyo kwanza ilikuwa inafanyiwa majaribio na hata kutoka Marekani haijatoka je, huo mzigo gani ilibeba?" Alihoji na kuongeza:

"Kuna watu wanapenda kuleta taharuki na kuchafua jina la Tanzania. Ndege yetu hii mpya haijatoka Marekani na wala haijagusa anga la Tanzania wanaanza kuleta uzushi usio na maana kwa nchi yetu," alisema Msigwa.

Ujio wa ndege hiyo ya mizigo utalifanya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kuwa na jumla ya ndege 12 ambazo zinafanya safari zake kwenye mikoa mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alisema hivi karibuni kuwa serikali iliamua kununua ndege hiyo baada ya kuona uhitaji mkubwa wa ndege ya mizigo.

Alisema ujio wa ndege hiyo ni ukombozi mkubwa kwa wafanyabiashara wa Tanzania na wageni ambao kwa muda mrefu wamekuwa na shauku ya kuona Tanzania inakuwa na ndege ya aina hiyo.

Kwa sasa shirika hilo linasafirisha wastani wa tani 3,000 kwa mwaka ambazo ni wastani wa kilo 3,000,000 za mizigo zinazoingia nchini na kutoka kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Mapema mwaka jana, Raymond Manyika wa Kitengo cha Mizigo (ATCL), aliliambia gazeti hili kuwa kwa wastani ATCL inasafirisha tani 250 ambazo ni sawa na kilo 250,000 kwa mwezi. "Kutoka China tunasafirisha sana vifaa vya kielektroniki, vipuri vya magari na nguo ambavyo wakati mwingine tunaingiza nchini na kusambaza kwenye nchi za Zimbabwe, Zambia, Uganda, Burundi na Sudan Kusini," alisema.

Alitaja mizigo mingine inayosafirishwa nje ya nchi hususani China ni mazao ya bahari kama ngadu, samaki wa mapambo wakati wanasafirisha sana maparachichi kwenye mji wa Mumbai nchini India.



# UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE

## VYA BAJETI VYA MWAKA 2022/23 NA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2023/24

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Nishati

DODOMA
MEI, 2023

## 1.0 UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2022/2023

# 1

**Kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwemo kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)*.**

### A. Uzalishaji wa Umeme:

1. Uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa umeongezeka kwa asilimia 10.5 na kufikia MW 1,872.05 ikilinganishwa na MW 1,694.55 za mwaka 2021/22.
2. Utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115, umefikia asilimia 86.89 ikilinganishwa na asilimia 60.22 za mwezi Aprili, 2022
3. Hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2023 kina cha maji ya Bwawa la JNHPP kilifikia mita 160.51 kutoka usawa wa bahari ambapo ili kuweza kuzalisha umeme, kiwango cha chini cha maji kinatakiwa kufikia mita 163 kutoka usawa wa bahari. Aidha, hadi kufikia tarehe hiyo, kiwango cha maji kilifikia mita za ujazo bilioni 11.8 sawa na asilimia 39.3 ya kiwango cha juu ambacho ni mita za ujazo bilioni 30.
4. Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185 umekamilika na kuchangia MW 185 katika Gridi ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huo mwaka 2021/22 ulikuwa asilimia 88.
5. Utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80 umefikia asilimia 99 ikilinganishwa na asilimia 91.6 za mwaka 2021/22.
6. Taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ya Kakono (MW 87) na Malagarasi (MW 49.5) zimekamilika.
7. Miradi mingine ya kuzalisha umeme, ikiwemo kwa kutumia maji ya Ruhudji – MW 358, Kikonge – MW 321 na Rumakali – MW 222 na kwa kutumia Jua mkoani Shinyanga – MW 150 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.



### B. Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme

1. Miundombinu ya kusafirisha umeme imeongezeka na kufikia jumla ya urefu wa kilomita 6,363.27 sawa na ongezeko la asilimia 4.1 ikinganishwa na kilomita 6,111.27 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022;
2. Miundombinu ya kusambaza umeme imeongezeka na kufikia kilomita 168,548.36 sawa na ongezeko la asilimia 9.5 ikilinganishwa na kilomita 153,988.49 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022;
3. Mradi wa Kusafirisha Umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze – kV 400 umefikia asilimia 93.5 ikilinganishwa na asilimia 44 mwaka 2021/22. Aidha, ujenzi wa kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze ambacho ni sehemu ya mradi huo umefikia asilimia 64 ikilinganishwa na asilimia 3.59 mwaka 2021/22.
4. Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi umekamilika. Utekelezaji wa mradi huo ulikuwa asilimia 99 mwaka 2021/22.
5. Utekelezaji wa mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga umefikia asilimia 95 ikilinganishwa na asilimia 79.3 mwaka 2021/22.
6. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi umekamilika, ambapo utekelezaji wake ulikuwa asilimia 79 mwaka 2021/22.
7. Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* umeendelea kutekelezwa kwa kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kupitia kituo cha Nyakanazi na kuunganisha Wilaya za Ngara na Biharamulo kwenye kituo cha Gridi ya Taifa Nyakanazi.
8. Serikali kupitia TANESCO inatekeleza jumla ya miradi 48 ikijumuisha miradi 20 ya kuongeza uwezo wa miundombinu ya usafirishaji umeme, miradi 12 ya kuboresha mifumo ya uendeshaji wa Gridi ya Taifa na miradi 16 ya ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji umeme.
9. Ilisainiwa mikataba 26 baina ya Serikali na Wakandarasi yenye thamani ya shilingi trilioni 1.9 ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kuimarisha Gridi ya Taifa.
10. Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi umefikia asilimia 26.7.



11. Serikali imetoa Shilingi bilioni 16.43 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 6,500 wanaopisha mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA) na Wananchi 4,750 tayari wamelipwa fidia zao.
12. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa ajili ya uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot II) umefikia asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 88 mwaka 2021/22.
13. Jumla ya wateja 4,319,258 wameunganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.4 ikilinganishwa na wateja 3,842,096 waliokuwepo mwezi Juni, 2022.
14. Miradi mbalimbali ya usafirishaji umeme, ikiwa ni pamoja na Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma na Tabora hadi Kigoma kupitia Urambo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

# 2

**Kutekeleza Miradi ya Nishati Vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika Vitongoji vyote nchini.**

1. Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round 2) umefikia asilimia 68.66 ambapo vijiji 1,880 kati ya 4,071 sawa na asilimia 46.18 vimeunganishiwa umeme na vijiji vyote Tanzania Bara vitakuwa vimeunganishiwa umeme ifikapo mwezi Juni, 2024. Hadi sasa jumla ya vijiji 10,127 vimeungiwa umeme sawa na asilimia 82 ya vijiji vyote.
2. Utekelezaji wa mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – *(Hamlet Electrification Project – HEP)* umeanza ambapo zoezi la kuwapata wakandarasi kwa ajili ya kupeleka umeme katika vitongoji 654 vilivyopo katika Mikoa ya Songwe na Kigoma lipo katika hatua za mwisho.
3. Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B unaolenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye vitongoji 1,686 katika mikoa ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe na kuunganisha jumla ya wateja wa awali 95,334 uliendelea kutekelezwa kwa Wakandarasi kufanya upimaji wa njia za ujenzi wa mradi, kuandaa michoro pamoja na ununuzi wa vifaa.
4. Taratibu za kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili C zilikamilishwa. Mradi huo unalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye vitongoji 1,880 katika mikoa ya Manyara, Iringa, Rukwa, Mtwara, Ruvuma, Simiyu na Mara kwa kujenga kilomita 6,562 za msongo mdogo na kufunga mashineumba 1,932 ili kuunganisha wateja wa awali 131,719.
5. Utekelezaji wa Mradi wa Peri Urban Awamu ya Pili ulifikia asilimia 91.0 ikilinganishwa na asilimia 84.4 mwaka 2021/22. Mradi huu unahusisha kupeleka umeme katika maeneo 153 yaliyopo katika majiji ya Arusha, Dodoma na Mwanza kwa kujenga miundombinu ya kusambaza umeme yenye urefu wa kilomita 751, kufunga mashineumba 143 na kuunganisha wateja wa awali 16,328.
6. Jumla ya mikataba nane (8) ilisainiwa na Wakandarasi watano (5) kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa Peri Urban Awamu ya Tatu katika mikoa nane (8) ya Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida Tabora na Tanga na wakandarasi hao wamekamilisha upimaji na usanifu na wanaendelea na kazi ya ununuzi wa vifaa na kuanza ujenzi wa miundombinu.
7. Serikali imepata waendelezaji sita (6) wa miradi ya kusambaza umeme kwa kutumia nguvu ya jua, itakayotekelezwa katika visiwa 36. Wakandarasi hao wanaendelea na Upembuzi Yakinifu, kuandaa Mpango wa Biashara, Vyeti vya Athari za Mazingira na Hati ya Kinga ya Malipo ya Awali *(Advance Payment Gurantee)*.
8. Umeandaliwa Mwongozo na Kanuni za Utoaji Mikopo kwa waendelezaji wa ujenzi wa vituo vidogo vya mafuta vijijini. Aidha, fursa za mikopo husika zimetangazwa na waombaji wanatakiwa kuwasilisha maombi hadi kufikia tarehe 30 Agosti, 2023.
9. Wamepatikana Wakandarasi wanne (4) kwa ajili ya kusambaza umeme katika Vituo vya Afya 66 na Pampu za Maji 333 vilivyopo vijijini katika mikoa 25 Tanzania Bara. Wakandarasi hao wamekamilisha usanifu wa mradi na kuendelea na ununuzi wa vifaa pamoja na kuanza ujenzi wa miundombinu ya mradi.
10. Jumla ya taasisi 43,925 zinazotoa huduma kwa jamii ikiwemo za Elimu, Biashara, Pampu za Maji, Vituo vya Afya na Nyumba za Ibada zimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na taasisi 40,408 mwaka 2021/22.
11. Wamepatikana wakandarasi kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo 336 ya wachimbaji wadogo wa madini, maeneo ya kilimo na viwanda katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara. Wakandarasi hao wanaendelea na zoezi la upimaji wa kina wa njia za kusambaza umeme na ununuzi wa vifaa.
12. Serikali imefanya utambuzi wa wigo wa mradi wa Kupeleka Umeme katika Shule na Mahakama za Mwanzo Vijijini ambapo jumla ya shule 729 na mahakama 292 zimebainishwa kuwa na uhitaji wa kuunganishiwa umeme. Aidha, REA na TANESCO wapo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kuanza utekelezaji wa mradi huu.
13. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini ikiwa ni pamoja na kuajiri Waratibu wa miradi ya nishati vijijini kwa Wilaya zote za Tanzania Bara; kutoa kibali cha kuajiri Wahandisi 20 wa miradi ya REA na kununua magari 21 yatakayotumika katika usimamizi wa miradi ya REA katika mikoa mbalimbali nchini.



## 3

**Kukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG Lindi na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake.**

1. Mazungumzo ya mradi wa LNG yamekamilika kwa kuandaliwa kwa Mikataba miwili mikubwa ambayo ni Mkataba wa Nchi Hodhi na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanywaji Mapato (PSA).
2. Serikali tayari imeanzisha Ofisi ya Mradi wa LNG kwa ajili ya kuratibu, kuwezesha na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya mradi kwa tija na ufanisi ili manufaa yake yapatikane kwa wakati kama ilivyokusudiwa.



## 4

**Kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya Nishati (*Energy Efficiency and Conservation*).**

1. Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kupitia jotoardhi ya Ngozi (Mbeya) - MW 70, Songwe (Songwe) - MW 5, Kiejo-Mbaka (Mbeya) – MW 60, Natron (Arusha) – MW 60 na Luhoi (Pwani) – MW5.
2. Umenunuliwa mtambo wa kuchoronga visima vya uhakiki (*drilling rig*) kwa miradi ya jotoardhi. Kupatikana kwa Mtambo huu kutawezesha uchimbaji kwa maeneo yote yaliyoainishwa kuwa na viashiria vya jotoardhi na kupata matokeo stahiki kwa haraka.
3. Bei elekezi za Kampuni sita (6) za wazalishaji wadogo wa umeme ziliidhinishwa. Bei hizi zinaendelea kuhamasisha na kuchochea uwekezaji binafsi katika uzalishaji umeme.
4. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, kulikuwa na jumla ya Wazalishaji Wadogo 17 waliozalisha jumla ya MW 70.17 kupitia vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu, ikiwa ni pamoja na tungamotaka, jua na mvuke.
5. Maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Nishati ya Tungamotaka yalianza kwa kukamilisha Hadidu za Rejea kwa ajili ya Mshauri Mwelekezi wa kuandaa Mkakati huo pamoja na kukusanya maoni ya wadau kuhusu masuala muhimu ya kuzingatiwa katika Mkakati huo.
6. Serikali ilianza kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati na uhuishaji wa Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati ili kuendana na mahitaji halisi ya matumizi bora ya nishati kwa sasa.

## 5

**Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, ikiwemo uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve*) na Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund - FPSF*).**

1. Nchi imeendelea kuwa na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta kwa kuhakikisha uwepo wa akiba ya mafuta ya kutosha.
2. Yaliwasilishwa Serikalini mapendekezo ya kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund*). Kwa sasa tathmini inaendelea kufanyika kuhusu vyanzo vya fedha za mfuko huo ili uwe endelevu kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa, pamoja na muda muafaka wa kuanzisha kwa kuzingatia mwenendo wa bei za mafuta katika soko la Dunia.

## 6

**Kuiimarisha TPDC na Kampuni zake Tanzu za TANOIL na GASCO.**

1. Serikali iliridhia kubadili mkopo wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba na Mitambo ya Kuchakata Gesi Asilia wa Dola za Marekani 1,193,611,687.49 kuwa mtaji wa Serikali kwa TPDC. Hatua hii itaimarisha Mizania ya Hesabu (Balance Sheet) za TPDC na hivyo kuliwezesha Shirika hilo kuvutia uwekezaji katika utafutaji na uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi na kuimarisha mapato.
2. Utendaji wa TPDC umeendelea kuimarishwa, ikiwa ni pamoja na kuunda Bodi ya Shirika hilo inayoongozwa na Balozi Ombeni Sefue (Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu), na kufanya mabadiliko makubwa kwenye menejimenti ya shirika hilo. Aidha, Serikali imeondoa menejimenti yote ya Kampuni tanzu ya TANOIL na kuteneza mkakati mpya wa biashara na uendeshaji wa kampuni hiyo.




## 7

**Kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na Ghala za dhamana ya forodha *(Customs Bonded Warehouse)* na Kituo cha Pamoja cha kupokelea Mafuta kutoka Melini *(Single Receiving Terminal)*.**

1. Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilisaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Kampuni ya ENOC LLC ya Falme za Kiarabu kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam. Aidha, tayari eneo la kujenga kituo hicho limepatikana na Serikali ilishaunda Kikosi Kazi kinachosimamia utekelezaji wa mkataba ulioingiwa.
2. Kampuni ya TIPER iliendelea na ujenzi wa matenki mawili yenye ukubwa wa lita milioni 30 kila moja ili kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi mafuta kama Kituo cha Kupokea Mafuta kwa Pamoja *(Single Receiveing Terminal - SRT)*. Aidha, TIPER iliendelea kusimika pampu za kuhamisha mafuta zenye uwezo wa kusukuma lita 800,000 kwa saa ili kuongeza kasi ya kuhamisha mafuta kwenda kwenye maghala ya Kampuni za Mafuta (OMCs).

## 8

**Kuimarisha utendaji wa taasisi za Wizara, hasa TANESCO, EWURA na PBPA, na huduma zinazotelewa na taasisi hizo.**

1. Serikali ilibadili madeni ya TANESCO yanayofikia Shilingi trilioni 2.4 kuwa mtaji wa Shirika hilo. Hatua hiyo itavutia uwekezaji pamoja na kuimarisha utendaji na mapato ya Shirika hilo.
2. TANESCO ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha utoaji wa huduma, ikiwemo kuwepo kwa kituo cha miito ya simu *(unified call centre)* ambacho kinafanya kazi saa 24; kuendelea kutumia mfumo wa maombi ya umeme wa Nikonekt ambao unawezesha wateja kuomba kuunganishiwa umeme hadi kufungiwa pasipo kufika ofisi za TANESCO; na kuanzishwa kwa mfumo wa Huduma ya Nihudumie ambao unatumika kuboresha huduma kwa wateja na kuwezesha utoaji wa taarifa kwa mteja kuhusu kushughulikiwa kwa suala alilowasilisha TANESCO hadi linapokamilika.
3. EWURA iliboresha mfumo wa *National Petroleum and Gas Information System* (NPGIS) unaowezesha Serikali kupitia Mamlaka hiyo kupata taarifa za hali ya upatikanaji wa mafuta nchini.
4. EWURA iliboresha mfumo wa kupokea maombi ya leseni za umeme, mafuta na vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta *(Licensing and Order Information System – LOIS)*.
5. Serikali imeunda Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA inayoongozwa na Prof. Mark Mwandosya (Waziri Mstaafu) pamoja na kuteua Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo.
6. EWURA imehuisha Kanuni mbili (2) za udhibiti, ambazo ni Kanuni ya Umeme ya Huduma za Ufungaji Mifumo ya Umeme – *The Electricity (Installation Services)* (*Amendment*) *Rules*, 2023 na Kanuni za Usimamizi wa Miundombinu na Biashara ya Mafuta - *The Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) (Amendment) Rules,* 2023. Lengo la uhuishaji huo ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa leseni na kuwezesha wananchi kumudu gharama za huduma.

## 9

**Kuongeza ushiriki na uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Nishati.**

1. Serikali kupitia TANESCO imesaini Hati za Makubaliano (*Memorandum of Understanding – MoUs*) na Kampuni binafsi mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu, gesi asilia na makaa ya mawe. Wawekezaji hao binafsi ni pamoja na: Total Eren (MW 200); Abu Dhabi FutureEnergy Company PJSC - Masdar (MW 2,000); Sumitomo (MW 300 – 600); Mbeya Power Ltd (MW 300) na Kilwa Energy (MW 318). Kazi za Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) zinaendelea kwa sasa ili Wawekezaji hao washiriki katika uzalishaji wa umeme.
2. Serikali imeanza taratibu za kuingia makubaliano na kampuni ya AFRICA50 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kwa mfumo wa wasafirishaji binafsi wa umeme *(Independent Power Transmission – IPT)*. Miradi hiyo ni Rufiji – Kibiti – Likong'o; Likong'o – Somanga Fungu; Mtwara – Tunduru – Songea; Segera – Same – Kisongo; na Kinyerezi – Somanga Fungu.
3. Serikali imeanza taratibu za kuingia makubaliano na wawekezaji binafsi ambao ni Larsen & Toubro Ltd na Gridworks Development Partners LLP kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Chalinze – Dodoma, Chalinze – Segera na Segera – Tanga pamoja na vituo vya kupoza umeme vyenye uwezo wa MVA 300 Segera, upanuzi wa kituo cha MVA 750 Dodoma *(bay extension)* na MVA 150 Tanga.
4. Serikali imeidhinisha bei elekezi za Kampuni sita (6) za wazalishaji wadogo wa umeme ambazo zinahamasisha na kuchochea uwekezaji wa Sekta Binafsi katika uzalishaji umeme. Kampuni hizo ni, Husk Power Limited, Watu na Umeme Tanzania Limited, POWERGEN Renewable Energy Limited, Jumeme Rural Power Supply, na POWERCORNER Tanzania Limited.
5. Wamepatikana waendelezaji watatu (3) wa miradi ya kusambaza umeme kwa kutumia nguvu ya jua katika visiwa 28 vilivyopo katika mikoa ya Kagera (8), Mwanza (13), Mara (3) na Lindi (4) na kuunganisha umeme kwa wateja 9,515
6. Serikali kupitia Wizara ya Nishati imesaini MoU na Kampuni ya ENOC LLC ya Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam

## 10

**Kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia unaimarika.**

1. Jumla ya Watanzania 1,969 waliajiriwa kupitia ajira za moja kwa moja na Watanzania 160 waliajiriwa kwa ajili ya uchukuaji data za mitetemo za mfumo wa 3D katika Kitalu cha Ruvuma. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, jumla ya Dola za Marekani milioni 134.6 sawa na Shilingi bilioni 313.14 zilitumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka soko la ndani.
2. Kampuni za ndani ziliendelea kutambuliwa na kusajiliwa katika Kanzidata ya *Local Suppliers and Service Providers* (LSSP) kwa ajili ya kupatiwa kipaumbele katika fursa zilizopo kwenye miradi mbalimbali hususan Mradi wa EACOP. Jumla ya Kampuni 1,748 zimesajiliwa katika kanzidata ambapo 190 zilipata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kwenye Mradi.
3. Kampuni ya kitanzania *(Solution Tag)* ilishinda zabuni ya kukagua na kusafisha bomba la gesi asilia (*intelligent pigging*) lenye urefu wa mita 800 linalotoa gesi asilia kutoka katika kisima hadi ulipo mtambo wa kuchakata gesi asilia wa Mnazi Bay. Kazi hii itahusisha vilevile kukagua na kusafisha bomba la kilomita 27 linalosafirisha gesi kutoka ulipo mtambo wa kuchakata gesi wa Mnazi Bay hadi kituo cha kupokea gesi asilia Mtwara mjini. Zabuni hii ina thamani ya takriban Dola za Marekani 500,000 sawa na Shilingi bilioni 1.6.

## 11

**Kufufua Shughuli za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia.**

1. Shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia zimeendelea katika vitalu vya Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi–Wembere, Songo Songo Magharibi, Ziwa Tanganyika na Vitalu Namba 4/1B na 4/1C.
2. Serikali inaendelea kudurusu Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji wa Mapato (*Model Production Sharing Agreement* - MPSA) wa mwaka 2013 ili kuwa na MPSA mpya inayoendana na mazingira ya sasa na itakayovutia uwekezekaji wa Sekta Binafsi katika utafiti na uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.
3. Serikali kupitia PURA inaendelea kuweka mipaka ya Vitalu vitakavyonadiwa na kuandaa Vifurushi vya Data *(Data Packages)* kwa kila Kitalu. Aidha, jumla ya Vitalu 26 vinafanyiwa uchambuzi ili kupendekezwa kuingizwa katika mnada, ambapo 15 vipo nchi kavu na 11 baharini.
4. Serikali kupitia PURA inatarajia kuendesha Duru ya Tano (5) ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kati ya mwezi Desemba, 2023 hadi Machi, 2024 baada ya kukamilika kwa shughuli za maandalizi zinazoendelea.
5. Serikali kupitia PURA imekamilisha uandaaji wa rasimu ya Ramani ya Kidijitali (*Interactive Digital Petroleum Reference Map*) kwenye Mfumo wa Taarifa wa Kijiografia (*Geographical Information System – GIS*) inayotoa taarifa za Vitalu vya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

## 12


**Kuongeza matumizi ya nishati ya gesi kwa kupikia (LPG) na kwenye magari na viwandani (CNG).**

1. Kumefanyika mjadala wa kitaifa wa Nishati safi ya kupikia tarehe 1 na 2 Novemba, 2022 na kwa sasa inakamilishwa Dira na Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia utakaozinduliwa mwezi Julai, 2023 na kuanza kutekelezwa
2. Serikali imetoa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa Taasisi za umma na Binafsi zinazolisha zaidi ya watu 100 kuanzia mwezi Januari, 2024 ili kuimarisha matumizi ya nishati ambayo ni rafiki wa mazingira, ikiwemo gesi.





3. Jumla ya leseni mbili (2) za kampuni za gesi ya LPG na leseni 19 za mawakala wa Gesi ya LPG zilitolewa.
4. Vimetolewa vibali vitatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kujaza gesi asilia (CNG) katika magari yanayotumia nishati hiyo kwa Kampuni ya Taqa Dalbit Jijini Dar es Salaam, TP Company Ltd Bagamoyo na Dangote Cement Limited Mkuranga mkoani Pwani.
5. Vimetolewa vibali vitatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa TPDC Jijini Dar es Salaam na Mnazi Mmoja Mkoani Lindi pamoja na Kampuni ya PanAfrican Energy Jijini Dar es Salaam.
6. Serikali kupitia REA imekamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayebainisha aina ya nishati safi itakayotumika katika maeneo ya Taasisi za Umma.
7. Taratibu za ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Pwani itakayounganisha wateja 980 wa awali zinaendelea.
8. REA ilitangaza fursa za usambazaji wa mitungi ya gesi kwa sekta binafsi.
9. REA inakamilisha Mwongozo wa Usambazaji wa Majiko Banifu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ambapo majiko 70,000 yatasambazwa katika maeneo ya vijiji na vijiji miji.
10. Ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia lenye urefu wa kilomita 12.4 kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach kupitia barabara ya Bagamoyo umefikia asilimia 44.2 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023.
11. Ujenzi wa bomba la kusambaza gesi katika maeneo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) na Mlimani City umeendelea ambapo migahawa mitatu (3) na maabara moja (1) katika chuo cha DUCE pamoja na migahawa kumi na mbili (12) iliyopo Mlimani City Mall itaunganishwa gesi.

### Ukuaji wa mahitaji ya umeme umeongezeka kutoka MW 832.55 mwaka 2010 hadi MW 1,431.59 Mwezi Mei, 2023




### Ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP), MW 2,115 umefikia asilimia 86.89, ikilinganishwa na asilimia 60.22 za mwezi Aprili, 2022





### Njia za Kusambaza Umeme Zimeendelea kuongezeka

| NA. | NJIA ZA USAMBAZAJI WA UMEME | UREFU (KM) | | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | | MEI, 2022 | MEI, 2023 | |
| 1. | Njia za msongo wa kV 33 | 48,965.73 | 55,045.55 | 12.4 |
| 2. | Njia za msongo wa kV 11 | 12,648.73 | 12,986.25 | 2.7 |
| 3. | Njia za msongo wa kV 0.4 | 92,374.03 | 100,516.56 | 8.8 |
| | **JUMLA** | **153,988.49** | **168,548.49** | **9.5** |

### Maboresho ya Huduma kwa Wateja pamoja na mambo mengine, yamewezesha kuunganisha umeme kwa jumla ya wateja 4,319,258 hadi Aprili, 2023 ambapo mwezi Juni, 2022 kulikuwa na wateja 3,842,096 walioungnishiwa huduma hiyo










### Mtambo wa kuchoronga visima vya uhakiki (drilling rig) kwa miradi ya jotoardhi umenunuliwa na kuwasili nchini



## 2.0 VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2023/24

| NA. | KIPAUMBELE KATIKA |
|---|---|
| 1. | Kupeleka umeme katika vitongoji 36,101 vilivyosalia, sawa na asilimia 56 ya vitongoji 64,760 vya Tanzania Bara. |
| 2. | Kukamilisha miradi ya uzalishaji wa umeme ikiwa ni pamoja na Miradi ya Umeme wa Maji ya Julius Nyerere (MW 2,115) na Rusumo (MW 26.67) pamoja na kutumia gesi wa Kinyerezi I Extension (MW 185). |
| 3. | Kuendelea kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme unaotokana na maji ikiwemo Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW 222), Kakono (MW 80), Malagarasi (MW 49.5); Kikonge (MW 300); umeme unaotakana na gesi wa Mtwara (MW 300), Mradi wa Mawe (MW 150) na Mradi wa Mwamba (MW 450) na miradi ya nishati jadidifu ya jotoardhi, upepo na jua. |
| 4. | Kukamilisha miradi mbalimbali ya usafirishaji wa umeme ambayo utekelezaji wake unaendelea. |
| 5. | Kuhakikisha umeme wa uhakika unaendelea kupatikana nchini kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika Mikoa ya Kagera na Katavi. |
| 6. | Kukamilisha Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu *(REA III, Round II)* ambapo umeongezwa wigo wa njia za Msongo Mdogo kutoka kilomita moja (1) hadi kilomita tatu (3) na wateja kutoka 22 hadi 66 kwa kila kijiji; pamoja na Miradi ya Ujazilizi Awamu ya IIA (Densification IIA) na Peri Urban II. |
| 7. | Kutekeleza mradi wa Ujazilizi Awamu ya IIB na IIC (*Densification IIB* na *IIC*); Peri Urban III; kusambaza umeme katika migodi midogo, maeneo ya kilimo na viwanda pamoja na kusambaza umeme katika maeneo yaliyo mbali na gridi *(off – grid projects)*. |
| 8. | Kuanza maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*, ikiwa ni pamoja na kufanya stadi za awali za utekelezaji wa mradi (*Pre-Front End Engineering Design – Pre-FEED)* na masuala ya kihandisi na kisanifu *(FEED)*. |
| 9. | Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda Hadi Tanga – Tanzania (EACOP); shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Kimkakati; usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na nchi jirani; kuimarisha matumizi ya CNG katika magari pamoja na kunadi vitalu (*licencing round*) vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini ili viendelezwe. |
| 10. | Kuendelea kutekeleza mikakati na programu mbalimbali za kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking)* nchini pamoja uanzishwaji wa vituo vidogo vya mafuta vijijini. |
| 11. | Kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia bidhaa hizo kwa kutekeleza mikakati mbalimbali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kwa manufaa ya walaji na uchumi kwa ujumla. |
| 12. | Kuendelea kuimarisha Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya TANESCO, TPDC, EWURA na PURA pamoja na Taasisi Tanzu ili yatoe huduma bora kwa mujibu wa matarajio ya wadau, kuimarisha mapato pamoja na tija na ufanisi katika uendeshaji. |
| 13. | Kuimarisha ushiriki wa wadau hususan Sekta Binafsi katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme, ikiwemo Kampuni za Africa 50, Gridworks na Larsen & Turbo na katika uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia. |
| 14. | Kuendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na rasilimali watu ya Wizara ya Taasisi zake na upatikanaji wa vitendea kazi muhimu. |

## 3.0 MIRADI YA KUZALISHA UMEME ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ILIYOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115. | Trilion1.5 |
| 2. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Ruhudji - MW 358. | Bilion 6.27 |
| 3. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Rumakali - MW 222. | Bilioni 5.2 |
| 4. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Kikonge - MW 330. | Milioni 500 |
| 5. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Malagarasi - MW 49.5. | Bilioni 15.52 |
| 6. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Kakono - MW 87.8. | Bilioni 36.53 |
| 7. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Jua wa Shinyanga - MW 150. | Bilioni 27.63 |
| 8. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Mawe - MW 150. | Bilioni 345 |
| 9. | Ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme cha Hale | Bilioni 6.4 |

## 4.0 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME ITAKAYOTEKELEZWA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ZILIZOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida-Arusha-Namanga. | Bilioni 15.91 |
| 2. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA). | Bilion 56.32 |
| 3. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Kigoma - Nyakanazi. | Bilion 34.00 |
| 4. | Ujenzi wa Kituo cha Kupooza Umeme Shinyanga | Bilioni 2.700 |
| 5. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Geita - Nyakanazi. | Bilioni 11.72 |
| 6. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco - Kyaka | Bilioni 5.800 |
| 7. | Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. | Bilioni 3.84 |
| 8. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere hadi Kituo cha Kupoza Umeme Chalinze. | Bilioni 20.50 |
| 9. | Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa (TANESCO Transmission Grid Rehabilitation & Upgrade Project –TTGRUP) | Bilioni 29.61 |

## 5.0 MIRADI YA KUSAFIRISHA UMEME ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTAYARISHAJI

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ILIYOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kV 400 Sumbawanga – Mpanda – Kigoma | Milioni 100 |
| 2. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma | Milioni 500 |
| 3. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Segera – Same hadi Lemugur (Arusha). | Bilioni 2.5 |
| 4. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme (Submarine Cable) Msongo wa kV 220 kutoka Tanzania Bara (Ununio) hadi Zanzibar. | Bilioni 2.35 |
| 5. | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Manyoni (Manyoni Substation – MVA 60) | Milioni 100 |
| 6. | Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Masaka - Ibadakuli) | Milioni 250 |

## 6.0 MIRADI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ZILIZOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II). | Bilioni 9.9 |
| 2. | Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – (*Hamlet Electrification Project – HEP*) | Bilioni 377.05 |
| 3. | Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili B. | Bilioni 24.76 |
| 4. | Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kusambaza bidhaa za Mafuta ya Petroli Vijijini. | Bilioni 10.00 |
| 5. | Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua kwenye Makazi Yaliyo Visiwani. | Bilioni 3.52 |
| 6. | Programu ya Kuwezesha Waendelezaji wa Miradi Midogo ya Nishati Jadidifu Vijijini chini ya Utaratibu wa Kusaidia Uandaaji wa Miradi (PPSF) | Bilioni 4.70 |
| 7. | Mpango wa Uendelezaji Miradi ya Nishati Jadidifu Inayofua Umeme kwa Kutumia Nguvu ya Maji. | Bilioni 5.0 |

## 7.0 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ILIYOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mnazi bay Kaskazini | |
| 2. | Eyasi - Wembere | |
| 3. | Songo Songo Magharibi | Bilioni 24.86 |
| 4. | Ziwa Tanganyika | |
| 5. | VitaluNa. 4/1B na 4/1C | |

## 8.0 MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA NA MAFUTA ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ZILIZOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG*). | Bilioni 6 |
| 2. | Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Ntorya (Kitalu cha Ruvuma) hadi Madimba. | Bilioni 58.75 |
| 3. | Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. | Bilioni 12.6 |
| 4. | Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Lindi na Mtwara. | Bilioni 1.6 |
| 5. | Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP) | Bilioni 70.2 |

## BAJETI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2023/24

Jumla ya Bajeti ni **Shilingi 3,048,632,519,000** ambapo:

A. **Shilingi 2,960,702,821,000** sawa na **asilimia 97.1** ya Bajeti yote ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mchanganuo wa:
   - » Shilingi 2,609,156,128,000 ni fedha za ndani; na
   - » Shilingi 351,546,693,000 ni fedha za nje.

B. **Shilingi 87,929,698,000** sawa na **asilimia 2.9** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa mchanganuo wa:
   - » **Shilingi 71,637,112,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); na
   - » **Shilingi 16,292,586,000** kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, akishiriki kufanya usafi pamoja na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiwanja cha Ndege, jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 5 mwaka huu, yatakayofanyika kitaifa mkoani Dodoma. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Jafo: Athari za mazingira zimeleta ukame, vifo mifugo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Selemani Jafo, amekiri kuwa athari za kimazingira nchini zimechangia kuwepo na ukame ambao umesababisha vifo vya mifugo, kupanda kwa bei za vyakula pamoja na mgawo wa maji na umeme.

Jafo, alisema hayo jana jijini hapa aliposhiriki tukio la upandaji miti katika Shule ya Sekondari Kiwanja cha Ndege ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani itakayofanyika Juni 5, mwaka huu.

“Hali ni mbaya sana maeneo ambayo yalikuwa yanapata mvua katika misimu miwili hivi sasa hakuna tena lakini pia kiwango cha mvua kimeshuka sana hali ambayo inasababisha ukame mkali,”alisema Jafo. Alisema, katika kipindi cha Agosti hadi Oktoba mwaka jana maeneo mengi yalikuwa na ukame mkali hali iliyosababisha vifo vya mifugo vilivyotokana na kukosekana kwa malisho pamoja na maji.

“Lakini pia ukame huu ulisababisha mgawo wa umeme kutoka na vyanzo vingi kupungua kina cha maji eneo kama Bwawa la Mtera ambalo tunalitegemea kwa ajili ya uzalishaji wa umeme takribani megawati 80 kutokana na ukame zilishuka hadi chini megawati 20. Kidatu pia megawati zaidi ya 204 zilishuka na kusababisha zaidi ya megawati 300 kuondoka kwenye gridi ya taifa”alisisitiza Waziri Jafo

Aidha, alisema athari hizo za kimazingira zimechangia kupanda kwa bei za vyakula ikiwemo unga wa mahindi kutoka na kukosekana kwa mvua na hata maeneo ilikonyesha ilikuwa ni chini ya wastani.

Kadhalika, Jafo alisema ili kukabilina na hali hiyo serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na athari hizo za kimazingira ikiwepo kuzindua kampeni ya upandaji miti pamoja na ile soma na mti katika shule za msingi na sekondari nchini.

“Nitoe shukrani kwa Rais wetu kuwa mfano na kuhamasisha utunzaji wa mazingira tangu akiwa Makamu wa Rais lakini pia Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, inaelekeza kila halmashari nchini kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka”alisema

Vile vile, Jafo aliagiza vibali vya ujenzi vinavyotelewa katika halmashauri nchini kuelekeza wamiliki wa maeneo kupanda miti kabla ya kuanza ujenzi ili kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za utunzaji wa mazingira.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema wameshiriki katika kampeni ya upandaji miti na kupiga marufu ya matumizi ya mifuko ya plastiki kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

## LATRA, mawakala mabasi kukutana kutatua kero

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) inatarajia kukutana na mawakala wa mabasi yaendayo mikoani wa Kituo Kikuu cha Mabasi Nanenane jijini Dodoma kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali zinazowakabili.

Moja ya kero zinazowakabili mawakala hao ni pamoja na kudorola kwa biashara ndani ya stendi hiyo kutokana na baadhi ya mabasi kutopakia abiria ndani ya stendi hiyo na badala yake hutumia vituo vingine vya nje.

Kero nyingine ni pamoja na kushindwa kuendesha ofisi walizopangisha katika eneo hilo kutokana na abiria kutoingia katika kituo hicho na kutumia vituo holela.

Akizungumza na Nipashe jana Ofisa Mfawidhi wa LATRA mkoani Dodoma, Ezekiel Emmanuel, alisema wamepokea barua ya malalamiko kutoka kwa mawakala hao na tayari wameanza kufanyia kazi kwenye vikao lakini pia wamepanga kukutana na halmashauri ya jiji kuona namna gani ya kutatua kero hiyo.

Alisema katika barua yao wamelalamikia baadhi ya vituo vinavyotumika kupakia abiria ambayo wanahitaji kujua kama vina vibali vya kufanya hivyo na kama havina basi utaratibu ufanyike wa kuwarejesha katika kituo hicho kikuu cha mabasi yaendayo mikoani.

“Ni kweli hizi changamoto wameziwasilisha ofisini nimeisoma barua yao na tayari nimeanza kuifanyia kazi, kinachotakiwa wavute subira ili kero hizo ziweze kutatuliwa,”alisema Emmanuel.

Hata hivyo alisema kuhusu suala la vituo hivyo ambavyo baadhi ya mabasi yanatumia kupakia abiria ni kazi ya halmashauri ya jiji hivyo watakapokutana moja ya suala ambalo litajadiliwa ili kulitafutia ufumbuzi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa mawakala wa mabasi wa kituo kikuu cha mabasi, Zakaria Mmari, alisema hali ya biashara hivi sasa ndani ya stendi hiyo imedorola kwa kiasi kikubwa kutokana na baadhi ya mabasi kutotumika kupakia abiria wake na badala yake hupakia katika vituo vya nje.

Mmari alivitaja baadhia ya vituo ambavyo vinachangia kupunguza abiria katika Kituo hiko ni pamoja na Kituo cha Mabasi cha CBE, Four Way, Ijenga, Magorofani, na Nzuguni. “Tunaiomba serikali iliangalie hilo vituo hivyo vinachangia hata utoaji tiketi zinazoandikwa kwa mkono ambazo serikali ilishazipiga marufuku,”alisema Mmari.

Naye Omary Haruna wakala wa basi la El -Saedy alisema baadhi ya mabasi kutopakia kwenye kituo hiko kunachangia kwa kiasi kikubwa kudorola kwa stendi hiyo ikiwemo kupoteza mapato.

Kutokana na hilo alisema wanamuomba Rais Samia kulingalia hilo ili waweze kuendesha biashara hiyo ambayo inachangia mapato serikalini.

# Mafundi mochwari Hospitali ya Manyoni wadai kutolipwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MAFUNDI na vibarua wanaojenga chumba cha kuhifadhia maiti wodi ya wanawake na wanaume katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida wamelalamika kutolipwa fedha zao hali iliyowafanya kukata tamaa kuendelea na mradi huo.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwa Katibu Tawala Mkoa wa Singida (RAS), Dk. Fatma Mganga alipofanya ukaguzi wa ujenzi wa majengo hayo na kubaini kusuasua kwa mradi huo.

Mafundi na vibarua hao walisema mkandarasi aliyepewa zabuni ya ujenzi wa mradi huo hawalipi fedha kwa wakati na pia anawalipa ujira mdogo kinyume na makubaliano na kumuomba Dk. Mganga kuingilia kati suala hilo.

Kutokana na malalamiko hayo, Katibu Tawala Mkoa wa Singida Dk.Mganga aliagiza kamati za ujenzi kukutana haraka na mkandarasi wa majengo hayo na kuwalipa madeni yao vibarua na mafundi wanaofanya kazi hiyo pamoja na kukaa mezani na kukubaliana malipo mapya ili kuondoa migomo baridi ya vibarua hao.

“Kila fundi anatakiwa kuwalipa vibarua wake kwa wakati na stahili walizokubaliana tofauti na hivyo itakuwa ni sababu ya ucheleweshaji wa kazi na tulishatoa maelekezo kwamba fundi mmoja jengo moja kama inawezekana mkandandarasi ashauriwe awaachie mafundi wengine jengo moja,” alisema.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya Manyoni Dk. Mwakafwila alimwahidi RAS kwamba atakutana na mkandarasi kujadili namna ya kuboresha ujenzi na suala la malipo ya vibarua ili ujenzi uweze kukamilika kabla ya Juni 30, mwaka huu. Katibu Tawala Mkoa wa Singida pia alitembelea mradi wa ujenzi wa Shule ya Msingi Eka iliyoko Kata ya Eka Wilayani Manyoni na kuwataka watendaji wa vijiji na kata kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu kazi ili fedha zilizotolewa zinatosheleze.

Hivyo, aliwagiza wasimamizi wa ujenzi wa miradi ya Boost mkoani hapa kuhakikisha mafundi wanakuwa na mipango kazi katika eneo la kazi itakayoonesha namna ya utekelezaji wa shughuli za kila siku tofauti na hivyo mafundi wataonekana wanafanya kazi kila siku lakini majengo hayaendelei.

Dk.Mganga alisema serikali kwa kiasi kikubwa imetambua umuhimu na mchango wa mafundi wa mtaani ndiyo maana imeendelea kuwapa kazi hivyo kuwataka kutopoteza imani hiyo kwa kufanya kazi nzuri, kutofanya uharibifu wa vifaa vya ujenzi na kubakiza kazi kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Awali aliwaeleza walimu katika miradi hiyo kuhakikisha wanapanda miti ya kivuko na matunda maeneo yanayowazunguka ikiwa ni pamoja na kuyapendezesha maeneo kwa kutengeneza bustani za maua.





Kamishina Msaidizi wa Polisi Wilaya ya Kinondoni, Ally Wendo, akizungumza na wakazi wa Kigogo jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, wakati wa kongamano la kupinga ukatili wa kijinsia lililoandaliwa na Taasisi ya Tanzania Ithna'ashariyah Community (TIC). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BRELA yazitaka mamlaka za kiuchunguzi kwenda kidijitali

**Na Nebart Msokwa**
MBEYA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni nchini (BRELA) imezitaka mamlaka za kiuchunguzi zilizoidhinishwa kupata taarifa za wamiliki manufaa wa kampuni kutumia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (ORS) ili kuzipata taarifa hizo kwa haraka na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Kwa mujibu wa BRELA matumizi ya taarifa za wamiliki manufaa ya kampuni kupitia mfumo wa ORS utaviwezesha vyombo vya uchunguzi kwenye utekelezaji wa mkakati wa taifa wa kudhibiti na kupambana na vitendo vya utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi pamoja na ufadhili wa silaha za maangamizi.

Mkuu wa Idara ya Usajili wa BRELA, Isdori Nkindi alibainisha hayo kwenye kikao cha majadiliano kuhusu utekelezaji wa kanuni za wamiliki manufaa baina ya wakala na vyombo vya uchunguzi kilichofanyika jijini Mbeya.

Nkindi alisema ofisi ya BRELA ilianza kutekeleza jukumu la kukusanya na kuzisajiri taarifa za wamiliki manufaa wa kampuni tangu Novemba 2021 na yenyewe kutoa urahisi wa kuzipata taarifa husika kwa vyombo vya kiuchunguzi vilivyoainishwa, vyenye mamlaka ya kufanya uchunguzi au upelelezi.

Alisema hadi sasa kumekuwa na maombi machache kutoka kwa mamlaka zilizoidhinishwa kupata taarifa hizo na ndiyo sababu BRELA ikaona umuhimu wa kuandaa vikao kwa ajili ya kuelimisha juu ya dhana hiyo pamoja na kujengeana uwezo wa kiutendaji hususani kwa taasisi zilizo na uwezo wa kupokea taarifa hizo kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

"Kama mnavyojua nchi yetu imeingia katika orodha ya nchi zisizo katika kundi la rangi ya kijani, tulikuwa kwenye kijani baadaye tukahama na ndiyo sababu uliandaliwa mkakati wa taifa wa kudhibiti na kupambana na utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi."alisema.

Pia alizisihi taasisi zote ambazo bado hazijawasilisha maombi kwa BRELA kwa ajili ya kupata uwezo wa kuingia kwenye mfumo wa ndani ikiwemo wa usajili kwa njia ya ORS kufanya hivyo ili kuliwezesha taifa kutekeleza mkakati iliyojiwekea.

Aliwataka pia wamiliki wa kampuni zilizosajiliwa kuendelea kuutumia muda waliopewa wa kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa ya kampuni akisema baada ya muda uliowekwa adhabu itakayoanza kutolewa ni kubwa na hawana sababu ya kutowasilisha taarifa hizo.

Mmoja wa washiriki wa kikao hicho, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Verus Rwetembula alipongeza BRELA kwa kuamua kukutana na wadau na kutoa ufafanuazi wa namna upatikanaji wa taarifa za kampuni na za wamiliki manufaa ya kampuni hizo.

Rwetembula alisema kwa wakala huo kuendelea kutoa elimu kwa wateja wake na taasisi zinazotakiwa kushirikiana kutawezesha taifa kufikia malengo ya kupambana au kukomesha vitendo vya uhalifu vinavyoweza kufanyika kupitia uwekezaji kwenye kampuni.

# Usimamizi mbovu chanzo ujenzi wa miradi mibovu

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

IMEELEZWA kuwa usimamizi mbovu wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali mkoani Mbeya ndiyo chanzo cha miradi hiyo kujengwa chini ya kiwango na hivyo kusababisha wananchi kukosa huduma.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo alipokuwa anafungua mkutano wa Taasisi ya Wahandisi Tanzania tawi la Mbeya na Songwe.

Mkutano huo ambao uliwashirikisha wahandisi, wanafunzi wa fani za kihandisi kutoka vyuo mbalimbali mkoani Mbeya ulikuwa na lengo la kutathimini kazi za kihandisi zinazofanyika.

Homera aliwataka wahandisi kuhakikisha wanafanya kazi kwa kuzingatia taaluma yao ili kuepuka kutekeleza miradi chini ya kiwango na hivyo kusababisha madhara kwa wananchi.

Alisema baadhi ya miradi ambayo imekuwa ikitekelezwa chini ya kiwango ni pamoja na madaraja, barabara, majengo na miradi mingine ambayo inahitaji wahandisi. "Taaluma yenu ni muhimu sana kwenye maendeleo ya taifa, huwa inasikitisha jengo linajengwa na injinia, mhandisi mshauri yupo lakini mradi baada ya muda mfupi unaharibika, nawaomba sana muwe mnazingatia sheria mnapofanya kazi zenu," alisema Homera.

Alisema makandarasi wazawa huwa hawapati tenda kubwa kwa sababu wengi wao huwa hawaaminiki na hivyo akawataka kutekeleza miradi vizuri ili warejeshe Imani.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Wahandisi mikoa ya Mbeya na Songwe, Mhandisi Memma Modu alisema mkutano huo ni sehemu ya shughuli zinazotakiwa kutekelezwa na taasisi hiyo katika kalenda ya mwaka.

Alisema kazi za kihandisi ni muhimu kwenye maendele ya nchi kwa maelezo kuwa shughuli zote za ujenzi zinategemea taaluma ya kihandisi.

Alisema wataendelea kushauliana ili kuhakikisha wanatekeleza miradi ya maendeleo vizuri na kupunguza malalamiko ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango. Hivyo, aliiomba serikali iendelee kuwaamini makandarasi wazawa kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa maelezo kuwa wanao uwezo wa kufanya kazi kama walivyo wageni.

# Wadau wahimizwa kushiriki kutokomeza udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU mkoani Mbeya wamehimizwa kuungana na serikali katika kupambana na hali ya udumavu hususani kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano kwa kushiriki kampeni mbalimbali za kuiwezesha jamii kutambua umuhimu wa lishe bora na upatikanaji wake.

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa 12 nchini iliyotajwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa mkoani Mtwara wakati wa kuwasha Mwenge wa Uhuru kuwa na kiwango kikubwa cha udumavu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa yenye kiwango cha juu na kwamba kwa sasa Mbeya ina kiwango cha asilimia 31.5.

Katika Kikao maalumu cha kujadili utekelezaji wa lishe katika Jiji la Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliwataka wadau wote kuungana na serikali ili kukabiliana na tatizo hilo ambalo linachafua taswila ya mkoa.

Miongoni mwa wadau aliosema ni muhimu kushiriki kwenye mapambano hayo ya udumavu ni pamoja na mashirika binafsi yanayojishughulisha na masuala ya kijamii ikiwemo afya na uchumi imara pamoja na taasisi zinazojikita kwenye shughuli za uzalishaji.

Aliwapongeza watendaji wa halmashauri na wadau wengine kwa kuanzisha mikakati ya kusaidia jamii maeneo ambayo serikali ilinakuwa imekwama ama inaendelea.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa wa shughuli za WeCare Foundation, Mkurugenzi wa shirika hilo, Elizabeth Maginga alisema katika kuimarisha malezi na makuzi ya awali ya mtoto wanashirikiana na wadau wengine wanaojihusisha na shughuli za kijamii zinazotoa huduma kwa watoto.

Alisema baada ya kufungua kituo cha mafunzo ya malezi na makuzi ya awali ya mtoto kwa wazazi na walezi katika Kituo cha Afya cha Aga Khan cha jijini Mbeya taasisi hiyo ina mpango wa kutoa huduma kama hiyo katika Hospitali ya Kanda ya Mbeya kitengo cha wazazi na wototo cha Meta.

Akizungumzia suala la lishe mkurugenzi huyo alisema kama wadau wakubwa wa malezi na makuzi ya awali ya mtoto wamejikita katika utoaji wa elimu ya lishe kwa wazazi na walezi sambamba na mama wajawazito kwakuwa wanaamini misingi ya ukuaji wa awali inaanzia tangu mtoto akiwa tumboni.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa mkakati wa lishe kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Ofisa Lishe wa Halmashauri hiyo, Itika Mlagila alisema pamoja na juhudi zilizofanyika tangu kuanza utekelezaji wa mkakati huo bado kuna maeneo yanayopaswa kutiliwa mkazo ili kuondokana na lishe duni.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala alitaka wadau wote kila mmoja kwa nafasi yake kutimiza yale yaliyo ndani ya uwezo.



# CCM yawaonya makada wake wanaoteta mitandaoni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, amewataka makada na wanachama wa chama hicho kutumia vikao vya chama kuwasilisha matatizo wanayoyaona kuliko kuongea kwenye mitandao ya kijamii maneno ambayo hayana taswira nzuri.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi kuu za CCM Kisiwandui baada ya kuwapo kwa taarifa katika mitandao ya kijamii ambazo zimetolewa na mwanasiasa mkongwe visiwani humo akikituhumu chama hicho.

Mbeto alisema chama kina utaratibu wake wa kuwasilisha taarifa ambazo zinahusu chama hicho kuliko kuongea hadharani.

Alisema chama kimepokea taarifa zilizotolewa na mmoja wa mwanasiasa kupitia mitandao ya kijamii, kwamba viongozi wa chama wanapaswa kulitafakari.

"Mtoa taarifa hizo ni mtu wetu katika chama wa siku nyingi na tunamuheshimu sana lakini nimuombe tu anapoona ana ushauri wowote kwa chama afike atapokelewa," alisema Mbeto.

Aidha, Mbeto alikanusha taarifa za mwanasiasa huyo alizotoa ya kwamba Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi hakuwa chaguo la chama akisema alipitishwa katika vikao halali vya chama na kuchaguliwa kwa kura nyingi.

Alisema tabia hiyo siyo nzuri na haikubaliki kichama, kwamba inaweza kusababisha mivutano na malumbano yasiyokuwa na sababu zozote zaidi katika kipindi hiki ambacho CCM ipo katika hatua ya kutekeleza ilani ya uchaguzi.

"Wakati wa mchakato wa kutafuta mgombea wa kiti cha urais kupitia chama hiki wanachama tofauti walijitokeza kuchukua fomu ya kugombea, mchakato wa mchujo ulifanyika na kupatikana wagombea watano ambao walifikishwa katika kamati kuu na hatimae Dk. Mwinyi ndiye alieibuka mshindi kwa kupata kura nyingi"alisema.

Hata hivyo Mbeto alisema miaka miwili ya uongozi wa Dk.Hussein Ali Mwinyi amefanikiwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia vizuri fedha za UVIKO -19 ambazo zimejikita katika ujenzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na hospitali 11 za Wilaya ya Unguja na Pemba.

Alisema CCM kinafurahishwa na utendaji wa uongozi wa Rais Dk.Mwinyi ambaye anachokifanya ni utekelezaji wa ilani ya chama hicho ya mwaka 2020-2025 na kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema matumizi mazuri ya fedha hizo katika sekta ya afya zimesaidia hospitali 11 za Wilaya ya Unguja na Pemba kujengwa na kukamilika kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema hospitali hizo zinakwenda kutoa jibu la kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vinavyotokana na kinamama na watoto ambapo malengo ni kuwawezesha wananchi kujifungua katika hospitali chini ya uangalizi wa madaktari wenye sifa.

Aidha, alisema katika sekta ya elimu tayari shule za msingi na sekondari 17 zimejengwa ambazo zitakwenda kupunguza msongamano wa wanafunzi.

Mbeto alisema mikakati ya serikali ni kuwawezesha vijana kupata ujuzi wa kazi za kujiajiri katika sekta ya elimu ambapo jibu pekee ni ujenzi wa shule za ufundi zitakazoibua vipaji.

Alisema: "CCM Zanzibar kimefurahishwa na kasi inayochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukifungua kisiwa cha Pemba katika ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano na barabara zinazokwenda vijijini pamoja na maeneo huru ya uchumi".



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohammed Said (kulia), akisalimiana na Mwakilishi wa jimbo la Mwera, Mihayo Juma Nhunga nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tanzania kuwatumia mabalozi wake kukuza kiswahili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) zimewasilisha mpango mkakati wa lugha ya kiswahili kuanza kutumika kwenye mikutano ya mabalozi wa Tanzania nje ya nchi kwa lengo la kuwahamasisha kufundisha na kueneza lugha hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Waziri huyo alikuwa akijibu swali la mbunge wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir, aliyetaka kujua serikali inazitumia vipi balozi kukikuza na kukieneza kiswahili duniani.

Akijibu swali hilo, alisema vitabu 210 vikiwemo cha mawasiliano ya msingi ya lugha ya Kiswahili kwa wageni na kamusi ya kiswahili fasaha wamepatiwa mabalozi ili viwasaidie kutumia kufundishia kiswahili katika vituo watakavyoanzisha katika balozi zao.

"Mheshimiwa Spika, Jumla ya nchi 13 hadi sasa zimeanza kutumia kiswahili kwa namna tafauti.

Nchi 10 kati ya hizo zinafundisha kiswahili kwa wageni kupitia diaspora zikiwemo Italia, Abudhabi, Korea ya Kusini, Uholanzi, Zimbabwe, Ufaransa, Cuba, Nigeria, Mauritius na Sudan,"alisema.

Aidha, alisema nchi mbili zina maktaba ya Kiswahili ambazo ni Afrika ya Kusini na Ujerumani na nchi moja ina klabu ya kiswahili ambayo ni Namibia.

Aidha, alisema baadhi ya balozi zimeanza kununua vitabu vya kiswahili katika mabaraza.

# Serikali: Mageuzi sekta ya elimu kutaongeza ufaulu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema mageuzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya elimu ikiwamo mitaala mipya na ujenzi wa shule 29 za msingi na sekondari kutasaidia kukuza na kuongeza ufaulu.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Lela Muhamed Mussa wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema Wizara imekuja na mageuzi mapya ambayo ni kuwepo kwa mitaala mipya ya elimu ya maandalizi na msingi ambayo sasa itatumika rasmi, hatua ambayo itasaidia kuwepo kwa kiwango cha ufaulu unaoridhisha.

Alisema mchakato wa mapitio ya mitaala ya elimu ya maandalizi na msingi yamepitia katika hatua mbalimbali ikiwemo kuwahusisha wataalamu wa sekta ya elimu pamoja na wananchi wa kawaida na wazazi.

Aliyataja mageuzi hayo yanahusisha na kupunguza masomo ya wanafunzi wa maandalizi na msingi ambapo kabla ya hapo masomo yalikuwa mengi kiasi ya kuwapa wakati mgumu wanafunzi na kuwatwisha mzigo mkubwa.

Alisema mtaala mpya wa elimu umejikita katika masuala ya kuwawezesha wanafunzi kupata huduma muhimu ikiwemo vitabu, kwamba tayari walimu 8,936 wa shule za serikali na binafsi wamepatiwa mafunzo ya awali juu ya mbinu ya matumizi ya mitaala hiyo.

"Mheshimiwa Spika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tumejipanga kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wetu ambapo matokeo yake ni kutayarisha mitaala mipya kwa wanafunzi wa elimu ya maandalizi na msingi ambao utaongeza ufaulu wa wanafunzi wetu na uwezo wa kuingia sekondari kwa mafanikio makubwa"alisema.

Aidha alisema serikali imepata mkopo nafuu wa Sh.bilioni 360 kwa ajili ya kufanya mageuzi makubwa ya sekta ya elimu katika visiwa vya Unguja na Pemba na kuleta ufanisi.

Aliyataja mageuzi hayo ni pamoja na kuimarisha elimu mjumuisho ambayo itayahusisha makundi yote ikiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalumu kufaidika na sekta ya elimu kikamilifu.

Mussa alisema Wizara ipo katika mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Elimu ya Zanzibar pamoja na sera yake ili kwenda na wakati wa mabadiliko ya ubora wa elimu yenye mabadiliko makubwa.

Aliyataja mageuzi ya sheria hiyo ni pamoja na kuona elimu inayotolewa iweze kuwaajiri wahitimu na kuingia katika soko la ajira moja kwa moja bila ya kutegemea ajira serikalini.

Alisema Wizara ipo katika hatua za mwisho za kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa wanafunzi wake ikiwemo kuziunganisha shule zote moja kwa moja na mkongo wa taifa kwa matumizi ya mawasiliano na teknolojia.

Alisema: "Hayo ndiyo mageuzi makubwa ya marekebisho ya Sheria ya Elimu na Sera ambayo tunatarajia kuyafanya. Tunataka kuona elimu yetu inakwenda kutoa ajira moja kwa moja kwa wahitimu wetu kuingia katika soko la ajira".

Pia aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha Sh.bilioni 457.2 kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

HABARI KITAIFA

## Jafo ajivunia mikakati imara kulinda mazingira

**Na Robert Hokororo,**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amesema Tanzania imeendelea kuweka mikakati na sera endelevu za uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira ikiwamo kuhamasisha upandaji miti ili kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Katika uzinduzi wa Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani jana jijini Dodoma, Dk. Jafo alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu, ajenda ya mazingira ni miongoni mwa vipaumbele muhimu vinavyoendelea kupewa msukumo na serikali ikiwamo uhamasishaji wa kampeni za usafi wa mazingira na upandaji miti.

Kwa mujibu wa waziri huyo, katika siku za hivi karibuni, Tanzania imeshuhudia athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi ambazo ziliathiri sekta mbalimbali za uchumi na uzalishaji mali na kushuhudiwa kuongezeka kwa bei za bidhaa za mazao ya chakula, hali iliyotokana na ongezeko kubwa la ukame katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Akifafanua zaidi, Waziri Jafo alibainisha kuwa baadhi ya maeneo yaliyopo katika visiwa vya Nungwi na Pemba, Zanzibar yameanza kushuhudia ongezeko kubwa la wingi wa maji ya bahari katika makazi ya wananchi hatua inayotokana na kuyeyuka kwa barafu na kusababisha kuongezeka kwa kiwango cha maji ya bahari.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali imeanisha mikakati, sera na vipaumbele mbalimbali vinavyolenga kuhamasisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira ikiwamo kuanzisha kampeni za upandaji miti, kutokana na ukweli kuwa hakuna mbadala wa mazingira katika mustakabali wa maisha ya binadamu na viumbe hai.

Alisema kila mwanadamu anahitaji mazingira safi na salama, hivyo kutokana na umuhimu huo katika kutekeleza kwa vitendo kaulimbiu ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Mwaka 2023, serikali imekuja na ajenda mahsusi kwa wananchi kwa kupanda miti na usafi wa mazingira katika maeneo nchini.

"Takribani miti milioni 276 itapandwa kila mwaka, na hili ni lengo la kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Kwa hapa Dodoma lengo ni kupanda miti milioni 40 ambalo ni lengo la kipekee kulinganisha na mikoa na wilaya zingine nchini. Tunazishukuru mamlaka za serikali za mitaa kwa kusimamia vyema kampeni hizi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule aliishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuendelea kuipatia ushirikiano ofisi yake na kutoa msukumo na hamasa ya uhifadhi wa utunzaji wa mazingira kupitia Mpango Mkakati wa Mazingira ambapo Mkoa wa Dodoma umetajwa kama mkoa pekee uliowekewa shahada ya uhifadhi wa mazingira.

# CCM yataka upanuzi uwanja wa ndege Nduli ukamilike ndani ya miezi minne

**Na Nebart Msokwa, IRINGA**

CHAMA cha Mapinduzi (CCM), kimeipa miezi minne Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kukamilisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Iringa 'Nduli' ili ndege kubwa za abiria na mizigo zianze kutua na kufungua fursa mbalimbali za kiuchumi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Aidha, kimeshauri jina la uwanja huo ubadilishwe na kuitwa Uwanja wa Kimataifa wa Mkwawa badala ya Nduli ili kumuenzi Shujaa wa Kabila la Wahehe, Chifu Mkwawa.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo aliyasema hayo jana alipotembelea uwanja huo kwa lengo la kuangalia maendeleo ya ujenzi ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake katika mkoa huo ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi, kusikiliza kero za wananchi na kukagua uhai wa chama.

Katika ziara hiyo Katibu Mkuu Chongolo aliongozana na viongozi mbalimbali wa chama kutoka makao makuu ya chama wakiwamo Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCM, Sophia Mjema, Katibu wa Oganizesheni, Issa Haji Ussi (Gavu) pamoja.

Alisema uamuzi wa serikali kuupanua uwanja huo ni kuuongezea hadhi ili wananchi wautumie kusafirisha mazao na bidhaa mbalimbali wanazozalisha kwenda kwenye masoko ya ndani na nje.

Alisema pia utasaidia kuongeza watalii kwenye vivutio vya watalii vilivyopo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Hifadhi ya Taifa ya Ruaha pamoja na maeneo ya kihistoria yaliyoko mkoani Iringa.

"Sasa naiagiza Wizara ya Ujenzi kuweka nguvu hapa ili kuhakikisha uwanja unakamilika na unaanza kutumika mapema, serikali kwa sasa imenunua ndege ya mizigo ambayo tunaamini itakuwa inasafirisha hata mazao ya wananchi wa maeneo haya," alisema Chongolo.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kujiandaa kunufaika na fursa za uwapo wa uwanja huo ikiwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara ambayo yatakuwa yanasafirishwa.

Akitoa taarifa ya upanuzi wa mradi huo, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mkoa wa Iringa, Mhandisi Batista Nyengo, alisema matengenezo ya uwanja huo yanahusisha njia ya kutua na kuruka ambayo itakapokamilika itakuwa na urefu wa mita 2,100 na upana wa mita 30.

Alisema mradi huo unatekelezwa na mkandarasi kampuni ya kichina, Sinohydro Corporation Ltd kwa gharama ya Sh. bilioni 63.7 na kwamba Mhandisi mwelekezi wa mradi huo ni Kampuni ya kihandisi ya TANROADS (TECU).

Alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti mwaka huu na mpaka sasa ujenzi wake umefikia asilimia 54.81 na kwamba kuna baadhi ya kazi hazikuwapo kwenye mkataba wa awali, lakini zimeongezeka.

"Mradi huu unagharimiwa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100 na mpaka sasa mkandarasi ameshawasilisha hati 13 za kuomba malipo zenye thamani ya Sh. bilioni 2,975 na ameshalipwa Sh. bilioni 24.9," alisema Nyengo.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alisema uwanja huo utakapokamilika utaunganisha hifadhi zote za taifa zilizoko kwenye mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema watalii watakuwa wanatua na ndege kwenye uwanja huo wanakwenda kutalii kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Kitulo kisha kwenda Katavi ama Morogoro na maeneo mengine.

Katibu Mkuu Chongolo alihitimisha ziara yake ya siku saba mkoani Iringa kwa kukagua miradi ya maendeleo, kusikiliza kero za wananchi na kisha kufanya vikao na viongozi wa chama kwa lengo la kupanga mipango mbalimbali ya chama.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2023, Abdallah Shaibu Kaim (wa tatu kushoto), akipokea maelezo ya ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji Mbweni kutoka kwa Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Kiula Kingu wakati mbio za Mwenge katika Wilaya ya Kinondoni mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Utekelezaji ushirikiano TCB, ALAT waanza

**Na Selemani Mpochi**

UHUSIANO wa kikazi kati ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB) na Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa (ALAT) umeanza kiuwezeshaji na ahadi za kushirikiana kibiashara ili kuisaidia serikali kutoa huduma kwa wananchi.

Wiki hii taasisi hizo mbili zimetamba zimejipanga vizuri kuunganisha nguvu zao kutimiza azma hiyo na ziko tayari kuhakikisha zinafanya kila linalowezekana kusaidia kuboresha maisha ya watanzania na kuchangia maendeleo ya kiuchumi nchini.

Kwa mara ya kwanza TCB imeshiriki mkutano mkuu wa mwaka wa ALAT ambao ulifanyika kwa siku mbili jijini Arusha kuanzia Jumatatu. Mbali na ushiriki huo, benki hiyo pia ilikuwa mmoja wa wadhamini wake kwa ufadhili wa Sh. milioni 100.

Benki ya TCB ilitumia fursa hiyo kujinadi si tu kwa washiriki zaidi ya 500 wa mkutano huo, bali pia kwa wajumbe wa ALAT na viongozi wa wanachama wa jumuiya hiyo ambao ni halmashauri zote 184 nchini.

Wakitoa maoni yao kuhuss ushirikiano huo, wana ALAT walisema hilo ni jambo jema na wako tayari kufanya kazi kwa karibu na TCB. Kufanya hivyo si tu ni jambo la kimaendeleo kwa taifa, bali pia la kizalendo.

Ni katika hafla iliyoandaliwa na TCB kama sehemu ya udhamini wake wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 37 wa ALAT uliofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC) na kufunguliwa rasmi Jumatatu na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Wajumbe wa mkutano huo, akiwamo Halima Mchoma, Diwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara, alisema kufanya kazi na TCB ni kusaidia kuiwezesha serikali, hasa kimapato.

Bahati Heneriko, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ya Kagera, alisema kufanya biashara na TCB pia kuna tija kimaslahi ya taifa kwa sababu ndiyo benki pekee inayomilikiwa kwa kiasi kikubwa na serikali.

Awali katika wasilisho lake Jumatatu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alisema wana mtandao wa tatu mpana wa matawi ambayo ni 82 nchi nzima yanayosaidiwa na ATM 86 na zaidi ya mawakala 5,000 kulihudumia taifa.

# MBEYA CITY YAMNYEMELEA MINZIRO, GEITA YAFAFANUA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuwa na msimu mzuri na Geita Gold FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Minziro, anatajwa kuwindwa na klabu mbalimbali za hapa nchini ikiwamo Mbeya City ya jijini, Mbeya.

Taarifa zilizopatikana zinasema Minziro ambaye sasa yuko Dar es Salaam kwa mapumziko mafupi, amemaliza mkataba wake na Geita Gold.

Akizungumza jana jijini, Minziro ambaye amewahi kuzifundisha timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Championship alisema kwa sasa yupo huru baada ya kumaliza mkataba wa miaka mitatu aliokuwa nao na Geita Gold.

"Tumeshamalizana, niko Dar es Salaam, nimemaliza mkataba wangu, kwa sasa nimepumzika kwanza nasikilizia, kama watanihitaji basi wataniita, wasiponihitaji basi, haya ni maisha, nitaangalia sehemu nyingine," alisema Minziro ambaye ndiye aliyeipandisha daraja timu hiyo kutoka Ligi ya Championship.

Kocha huyo alikiri amepata ofa kutoka timu mbalimbali ambazo zimeonyesha nia ya kuhitaji huduma yake kwa ajili ya msimu ujao.

"Siyo Mbeya City tu, zipo timu nyingi ambazo siwezi kuzitaja hapa, Mbeya mimi nimeshakaa sana wakati huo naifundisha Prisons, kwa misimu miwili nipo na Geita Gold na nimeifikisha kwenye nafasi ya sita mpaka sasa si jambo dogo na msimu uliopita niliifikisha nafasi ya nne na tukacheza mechi za Kombe la Shirikisho, unaweza kuona hapo," alisema beki huyo wa zamani wa pembeni wa Yanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Naye Mwenyekiti wa Geita Gold, Contastine Morandi, alisema wanaendelea na mazungumzo na Minziro na yanalenga katika kuboreshea mkataba wake, ingawa hawawezi kumzuia kama ataamua vinginevyo.

"Tuko katika mazungumzo ya kumwongezea mkataba, lakini unajua binadamu tena, kila mtu ana utashi wake, kama akikubali kuendelea na sisi hatuna shida kwani tunataka asalie katika kikosi chetu, lakini huwezi kujua moyoni mwake anafikiria nini," alisema Morandi.

Geita Gold iko katika nafasi ya sita ya kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 37, imebakisha mechi dhidi ya Ihefu na Mtibwa Sugar.




Wanachama wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), na wadau wengine wakishiriki jogging kama sehemu ya kampeni iitwayo 'Unga tela, vunja ukimya, safiri salama bila rushwa ya ngono inawezekana' yenye lengo la kupinga rushwa ya ngono iliyofanyika Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Prisons yasaka straika, beki

**Na Saada Akida**

WAKATI mabosi wa Tanzania Prisons wakisema timu yao iko tayari kuvuna pointi sita katika mechi mbili za Ligi Kuu Bara zilizobakia, pia wanahitaji kusajili wachezaji wapya watatu ili kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu mpya, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Tanzania Prisons, Enock Manguku, alisema wanahitaji kusajili straika, beki wa kati na kiungo moja ili kukiongezea nguvu kikosi chao kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao.

Manguku alisema kwa sasa wanaendelea na mipango ya kuinusuru timu hiyo isishuke daraja lakini wameshaanza kufanyia kazi mapendekezo yaliyowasilishwa na benchi la ufundi la timu hiyo.

"Tulikutana na kocha wetu Bares (Mohammed Abdallah), tumezungumza naye kuelekea mechi mbili zilizosalia pamoja na mipango yake kwa ajili ya msimu ujao, ametaja nafasi tatu za usajili ambazo ni mshambuliaji, beki wa kati na kiungo wa juu.

Tayari ametutajia majina na wengine nafasi zao, tumeanza kuifanya kazi kwa kuzungumza na nyota hao ambao majina yao yako mezani mapema sana, hatuwezi kuyataja kwa sababu wengine bado wanatumikia klabu zao na mikataba yao inafikia ukingoni msimu huu," alisema Manguku.

Aliweka wazi hawatafanya mabadiliko yoyote katika benchi la ufundi ambalo liko chini ya Bares ambaye bado ana mkataba na klabu hiyo.

"Tutakuwa viongozi wa ajabu sana kumwondoa kocha ambaye alitutoa katika nafasi ngumu na kutuweka nafasi yenye uhakika wa kuendelea kubaki kwenye ligi, tulishaongea naye na baada ya mechi yetu dhidi ya KMC FC tutakutana naye kwa ajili ya kupokea ripoti yake," alisema Manguku.

## KMC FC kuikabili Prisons bila Ame

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji 24 wa KMC FC kimewasili mjini Sumbawanga tayari kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Prisons itakayochezwa Juni 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mkoani, Rukwa.

Mechi ya Prisons imehamishiwa Sumbawanga ili kupisha sherehe za ubingwa wa Ligi Kuu ambazo zitafanyika baada ya kumalizika kwa mchezo kati ya Mbeya City dhidi ya Yanga.

Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, alisema kikosi hicho kiliondoka bila nyota wake wanne ambao ni majeruhi akiwamo beki wao kisiki, Ibrahim Ame.

"Tumekuwa na changamoto ya baadhi ya wachezaji majeruhi, daktari ametoa mapendekezo haina sababu ya kuwasumbua, ligi inakwenda ukingoni wapumzishwe tu ili wawe fiti kuanza kuitumikia KMC msimu ujao," alisema Mwagala.

Aliongeza wanatarajia mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa kwa sababu timu zote mbili bado hazijawa na uhakika wa kubakia katika Ligi Kuu au kuepuka kucheza 'play off', hivyo wamejipanga kupambana kusaka ushindi.

## Gofu Gymkhana, Lugalo kuchuana

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI wa gofu wa Jeshi la Wananchi la Lugalo wanatarajia kuchuana na wenzao wa klabu ya Gymkhana Dar es Salaam katika shindano litakalofanyika kesho hapa jijini, imefahamika.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Ofisa Habari wa klabu ya gofu ya Lugalo, Meja Selemani Semunyu, alisema wachezaji wao wamejipanga vyema kuelekea shindano hilo.

Semunyu alisema lengo la kuandaa shindano hilo ni kuimarisha na kujenga ushirikiano kati ya klabu hizo za gofu zilizo Dar es Salaam.

"Kwa upande wetu tumejipanga vizuri, tunataka tuwaonyeshe wenzetu wa Dar Gymkhana kuwa hatuna masiala tunapokuwa uwanjani," alisema Semunyu.

Aliongeza anaamini nyota wa Lugalo wataonyesha ubora wao na amewataka wadau kutoka sehemu mbalimbali kuendelea kujitokeza katika mchezo huo na kusisitiza si wa watu wenye fedha pekee kama inavyodhaniwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE YAMBAKISHA BRUNO

NEWCASTLE United imempa Bruno Guimaraes mkataba mpya wenye mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki ili asiende Liverpool, Real Madrid au Barcelona, timu zinazomtaka kiungo huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 25 na kumfanya awe mchezaji anayelipwa zaidi klabuni hapo. ***(Sun)***

### ALLISTER ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo katika mazungumzo na kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister, mwenye umri wa miaka 24, kuhusu maslahi binafsi na wanatarajia kukamilisha usajili wake kutoka Brighton wiki ijayo. ***(Fabrizio Romano)***

### JOAO KUTUA NEWCASTLE

JOAO Felix atapelekwa Newcastle United kwa mkopo na klabu mama Atletico Madrid siku chache tu baada ya Chelsea kutangaza kutomsajili mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno mwenye umri wa miaka 23 kwa uhamisho wa kudumu. ***(Mail)***

### CHEEK KUONDOKA CHELSEA

MCHEZAJI Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 27 amekubali kuondoka Chelsea na kwenda AC Milan huku klabu hiyo ya Ligi Kuu Italia, Serie A, ikitayarisha ofa ya pauni milioni 13 kwa kiungo huyo wa kati wa England. ***(La Gazzetta dello Sport via Sun)***

### KANE AITAKA UNITED

NAHODHA wa England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, anataka kuhamia Manchester United msimu huu wa joto, badala ya kuhamia nje ya nchi, lakini yuko tayari kumaliza mkataba wake na kuondoka Tottenham Hotspur kama mchezaji huru mwaka ujao. ***(Sun)***

### KANE ATAJWA MADRID

REAL Madrid inaweza kumnunua, Harry Kane, iwapo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Karim Benzema, mwenye umri wa miaka 35 atakubali ofa nono aliyotangaziwa huko Saudi Arabia. ***(Times)***

### SPURS YAMFUATA POSTECOGLOU

KLABU ya Tottenham Hotspur itaongeza harakati za kumnunua, Ange Postecoglou, baada ya timu yake ya Celtic kucheza fainali ya Kombe la Scotland hapo kesho. ***(Evening Standard)***

### CHELSEA KUMUUZA KOULIBALY

CHELSEA inataka kumuuza beki wa kati wa Senegal, Kalidou Koulibaly, mwenye umri wa miaka 31, ambaye alisajiliwa kwa pauni milioni 33 kutoka Napoli msimu uliopita wa joto. ***(Evening Standard)***

### KOVACIC ANUKIA CITY

CHELSEA pia imetoa ruhusa kwa Manchester City kuanza mazungumzo na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Croatia, Mateo Kovacic, mwenye umri wa miaka 29. ***(Mail)***

### PAVARD AGOMBEWA ULAYA

MANCHESTER United, Barcelona na Inter Milan zimeonyesha nia ya kumsajili beki wa pembeni wa Ufaransa, Benjamin Pavard, mwenye umri wa miaka 27, ambaye hataki kuongeza mkataba mpya na Bayern Munich. Mkataba wake wa sasa unakakamilika mwakani. ***(L'Equipe)***

### SALIBA MSHAHARA MNONO

ARSENAL imetoa ofa ya kuongeza mshahara wa William Saliba mara tatu zaidi katika mkataba mpya ambao utamfanya kupokea pauni 120,000, ingawa beki huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22 anawaniwa pia na Paris St-Germain. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO: SIFAHAMU HATIMA YANGU ROMA

●●●Ni baada ya kupata kipigo cha kwanza katika fainali ya Ulaya...

**ROME, Italia**

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho amesema hana uhakika kuhusu mustakabali wake katika klabu hiyo baada ya kufungwa kwa penalti 4-1 katika mechi ya fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla iliyochezwa juzi.

Kipigo hicho kilimaanisha Roma kushindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa msimu ujao na kuzua maswali iwapo kocha huyo mwenye umri wa miaka 60 atasalia katika mji mkuu wa Italia, baada ya kuhusishwa na Paris Saint-Germain.

"Lazima nipigane kwa ajili ya vijana hawa na kwa hiyo nisiseme kwa hakika nitabaki," alisema Mourinho, ambaye timu yake ilitoka sare ya 1-1 na Sevilla baada ya muda wa ziada, akiiambia Sky Sports Italia.

"Nilizungumza na klabu Desemba. Sijawasiliana na mtu mwingine yeyote tangu wakati huo. Nimebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wangu na hii ndio hali."

Kilikuwa ni kipigo cha kwanza kwa Mourinho katika fainali ya Ulaya, lakini alisema anajivunia uchezaji wa timu yake na kukiri msimu huu ulikuwa na matokeo mabaya.

"Tumechoka kimwili, tumechoka kiakili, tunahisi kufa kwa sababu tunaamini ni kushindwa bila haki na matukio mengi yanayoweza kujadiliwa," aliongeza kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Manchester United.

"Tumekufa tumechoka, lakini tunajivunia, huwa nasema unaweza kupoteza mechi ya mpira, lakini kamwe sio utu au taaluma yako.

"Nilipoteza, lakini ninarudi nyumbani nikiwa na furaha zaidi wakati huu. Vijana hao walitoa kila kitu msimu huu."

Mourinho pia alimkosoa mwamuzi, Anthony Taylor, akiongeza Mwingereza huyo alionyesha kadi nyingi za njano.

"Ulikuwa mchezo mkali, wa kiume, wa kusisimua na mwamuzi ambaye alionekana kuwa Mhispania. "Ilikuwa ya njano, njano, njano wakati wote," alisema. "Tumezoea ushawishi wa waamuzi katika michezo yetu, sio jambo jipya, lakini sikutarajia katika fainali ya Europa."



# MAGUIRE KUZUNGUMZA NA HAG KUHUSU HATIMA YAKE

**MANCHESTER, England**

HARRY Maguire atafanya mazungumzo na Erik ten Hag kujadili mustakabali wake ndani ya Manchester United baada ya mwisho wa msimu huu, vyanzo vimeiambia ESPN.

Maguire amevumilia kampeni ya kufadhaisha kwenye Uwanja wa Old Trafford, na kuanza mara 16 tu katika mashindano yote na mara nane pekee kwenye Ligi Kuu England.

Baada ya kuwa nyuma ya Lisandro Martinez na Raphael Varane katika nafasi ya beki wa kati, Maguire anatazamiwa kutathmini chaguo lake kabla ya kufanya uamuzi kuhusu wapi atacheza msimu ujao.

Vyanzo vimeiambia ESPN United iko tayari kusikiliza ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 huku West Ham United ikionyesha nia ya kumtaka.

Ten Hag yuko tayari kumbakisha Maguire kama sehemu ya kikosi chake lakini anaelewa mlinzi huyo wa England anaweza kutafuta kuondoka ili kupata sehemu ya kucheza zaidi.

Maguire ameitwa katika kikosi cha England kwa ajili ya mechi dhidi ya Malta na Macedonia Kaskazini Juni hii, lakini alipoulizwa kuhusu kukosa muda wa kucheza United, Kocha, Gareth Southgate alisema kwa uwazi "sio hali inayoweza kuendelea milele."

Maguire ana mkataba pale Old Trafford hadi mwaka 2025 pamoja na chaguo la mwaka mwingine, na United itatafuta ada kubwa kwa mchezaji aliyesajiliwa kwa pauni milioni 80 kutoka Leicester City mwaka 2019.

# Messi kuamua hatima yake

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi anatarajia kufanya uamuzi wa wapi atakwenda kucheza katika msimu ujao, wakati wowote kuanzia sasa, lakini inatajwa sehemu ambayo haifikirii ni kurejea Barcelona.

Hata hivyo kwa muda mrefu Messi ametajwa hana mahali kwingine ambapo atarejea zaidi ya Barcelona kwa sababu ndio timu ya ndoto yake na alitua hapo tangu akiwa na miaka 12 alipoondoka Argentina.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 35 na mshindi wa Kombe la Dunia bado anataka kubakia Ulaya, lakini baada ya kufanya uamuzi wa kuondoka Paris St-Germain katika msimu wa joto, hajapata ofa nyingi za kuvutia kutoka katika bara hilo.

Tayari maofisa wa serikali ya Saudi Arabia wameanza kufanyia kazi mchakato wa vibali cha mchezaji huyo kutua nchini humo.

Inaelezwa tayari Messi ameshafikia makubaliano binafsi ya ofa kutoka Al-Hilal na ameanza kujiandaa kutua katika klabu hiyo, ikitaka ni mahali panapomvutia mchezaji huyo.

Klabu ya Inter Miami ya Marekani pia inatajwa ni chaguo lingine la nyota huyo, ingawa ofa ya mkataba wa mkopo wa klabu hiyo na Barcelona, hazijawa pendekezo lake.



# City yajitosa kumwania Kovacic



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City ipo katika mazungumzo ya kumsajili, Mateo Kovacic, kutoka Chelsea, vyanzo vimeiambia ESPN.

ESPN iliripoti Februari kiungo huyo wa kati wa Croatia alikuwa mmoja wa wachezaji kadhaa ambao huenda wakapatikana huku Chelsea ikipanga kuwachia nyota wake wengi majira ya joto ili kupunguza kikosi chao kilichojaa na kocha mpya, Mauricio Pochettino.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake na hakuna mazungumzo yoyote ya maana juu ya kuongezwa kwa mkataba mpya.

Ingawa hakuna ada ambayo bado haijakubaliwa, vyanzo vinadokeza Kovacic amepewa ruhusa ya kujadiliana na City na Chelsea wanafikiriwa tayari kumwachia kwa ada ya pauni milioni 35.

Kocha wa City, Pep Guardiola anahitaji kuimarisha safu yake ya kiungo kabla ya msimu ujao.

Inaonekana kama Ilkay Gundogan atajitoa kwa City na mkataba wake unamalizika mwishoni mwa Juni huku Barcelona na Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazomvutiwa iwapo ataamua kuondoka lakini Kovacic angekuwa mbadala muhimu kutokana na uzoefu wake akiwa na Chelsea, Real Madrid na Inter Milan.

HABARI MICHEZO

# FEI TOTO ASISITIZA HATAKI KUREJEA KUCHEZA YANGA

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Feisal Salum 'Fei Toto' amesema hayuko tayari kurejea Yanga endapo kesi yake aliyoifungua katika Mahakama ya Usuluhishi ya Kimataifa (CAS), itagonga mwamba.

Fei Toto anajiandaa kwenda CAS baada ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kuamua mchezaji huyo anatakiwa arejee katika klabu yake ya Yanga.

Mabingwa hao pia walimtaka Fei Toto arejee klabuni ili wakae mezani kwa kuboresha maslahi yake au klabu inayomhitaji kuwasilisha ofa rasmi, lakini Mzanzibari huyo ameendelea na msimamo wake.

Akizungumza katika mahojiano jana, Fei Toto, alisema mchakato wa kwenda CAS umeshaanza na tayari ameshalipa kiasi cha fedha nusu ili shauri lake analohitaji lifanyiwe kazi.

Fei Toto alisema endapo pia atashindwa kupata haki yake huko basi yuko tayari kutocheza soka na si kurudi ndani ya kikosi cha Yanga ambayo inaongozwa wa Rais Injinia Hersi Said kwa sababu ya kumkosea mara kadhaa.

"Mimi natamani jambo hili liishe hata leo (jana), lakini nafsi yangu haipo tayari kurudi tena Yanga, hata kama kuna gharama za kulipwa nipo tayari najua ndugu zangu Watanzania hawawezi kuniangusha, nitaomba wanichangie na ikibidi hata kukopa ili niwe salama. Lakini kama itatokea sitocheza tena mpira nipo tayari sio kurudi Yanga kutokana na mambo niliyopitia.

Mimi tatizo langu kubwa ni Rais wa timu (Hersi Said), ndio maana nilipokaa naye chini nilimweleza naomba tumalizane ili kila mmoja aendelee na mambo yake, na mimi niendelee na maisha yangu. Kama Hersi akiondoka Yanga, hata leo sasa hivi nipo tayari kurudi Yanga, sina tatizo na klabu wala mashabiki," alisema Fei Toto.

Kiungo huyo alisema anawapenda mashabiki wa Yanga na anawapa pole maana hawajui kilicho nyuma yake.

"Nimeondoka Yanga kwa sababu ya manyanyaso, niliambiwa nimeuza mechi, nikaambiwa kama sitaki kucheza mpira nirudi kwetu Pemba, nilivumilia hata mama yangu alikuwa anadhalilishwa , alikuwa akinipa sana moyo, lakini pia ni shabiki mkubwa wa Yanga," alisema nyota huyo.

Naye wakili anayemsimamia kiungo huyo, Jasmin Razack, alisema mchakato wa kwenda CAS umeshaanza.

"Gharama za CAS ni kubwa sana, hadi sasa tumeshapata Sh. milioni tisa, bado watu wanaendelea kuchangia, sasa hivi Fatma (Karume) yuko Marekani na yeye huko anaendelea na mchakato wa kuchangisha ili tufanikiwe kwenda kufungua shauri letu," alisema Jasmin.

Alisema mchezaji wa kigeni anapokuwa na shida wanaenda FIFA ambako ada zake sio ghali kama CAS ambao linawasaidia changamoto za wachezaji wa ndani na naomba serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuliangalia zaidi jambo hili ili kuwasaidia nyota wa Kitanzania.

# Yanga yafunguka hapatoshi Algeria

INATOKA UK. 24

Karia. Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema maandalizi yote yamekamilika na kilichobaki ni kumalizia dakika 90 zilizobaki na kuongeza katika mechi ya kwanza wachezaji walikuwa na homa ya mchezo kitu kilichosababisha wapoteze.

"Tumeondoka na wachezaji wote, tumeondoka na kila silaha ambayo inatakiwa tuitumie kwenye mchezo huo, nadhani kitu ambacho kilitufanya tupoteze mchezo uliopita ni homa ya fainali, taasisi yetu ilikuwa haijawahi kupitia changamoto hiyo, hii ni mara ya kwanza kufika fainali ya Kombe la Shirikisho, wachezaji wetu wengi nao walikuwa hawajawahi kufika hatua hii, homa ikatuingia, presha ikawa kubwa, tukacheza kwa msukumo mkubwa, lakini kwa sasa hata ukizungumza na wachezaji wanakwambia wapo tayari kwenda kuifanya kazi," Kamwe alisema.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Yanga ilifungwa mabao 2-1, bao pekee la Yanga likifungwa na mshambuliaji wake tegemeo Mkoangomani, Fiston Mayele.

Ili kutwaa taji na kuweka rekodi ambayo Watanzania wanaisubiri kwa hamu, Yanga inatakiwa kupata ushindi wa kuanzia mabao 2-0.

Imeandaliwa na Adam Fungamwango na Romana Mallya, DODOMA



Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa Juni 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga. **PICHA: MTANDAO**

# Maandalizi fainali Kombe FA Tanga yameiva

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesema maandalizi ya mechi ya fainali ya Kombe la FA inayotarajiwa kufanyika Juni 12, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga yamekamilika.

Fainali ya mashindano hayo itamkutanisha bingwa mtetezi, Yanga dhidi ya Azam FC, zote kutoka Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Salum Madadi, maandalizi yote ya msingi yako tayari na shirikisho hilo linawakaribisha wadau wa soka nchini kushuhudia fainali hizo ambazo msimu huu zitafanyika kivingine.

Alisema lengo la fainali hizo kuchezwa Jumatatu ni kutaka kwenda na ratiba ya FIFA, licha ya kuingilia siku moja kutokana na kubanwa na ratiba ya wawakilishi wa Tanzania waliokuwa wanashiriki mashindano ya kimataifa, ambayo msimu huu tumeshuhudia Yanga ikifika fainali ya CAF.

"Mipango yetu tulipanga fainali iwe ndani ya kalenda ya FIFA kwa sababu klabu zilizoingia fainali kupata wachezaji wake wote kushiriki katika fainali hiyo, tulihofia nyota wakigeni wangweza kuitwa katika timu zao za Taifa. Safari hii tuzo tunaenda kufanyia nyumbani kwa TFF, tutatoa fursa ya watu kuona uwekezaji mkubwa uliofanywa na shirikisho hilo badala ya ule uliofanya Kigamboni," alisema Madadi.

Aliongeza anaimani matukio yote yatakayofanyika Tanga yatakuwa yakuvutia kwa sababu itakuwa ni fainali ya kipekee kutokana na ushindani wa timu hizo huku Yanga ikiwa imetoka katika fainali za Kombe la Shirikisho Afrika.

# Simba SC yajipanga kutorejea kinyonge

INATOKA UK. 24

inajulikana hata Brazil wanaizungumzia Simba, Mali, kila kona sasa tukiwa na wachezaji wazuri na wenye uwezo itakuwa rahisi kutupa matokeo na kuleta ushindani, tumekuwa na mwendo ambao umekuwa mzuri lakini sio kwa kiasi kikubwa hii ilitokana na wachezaji wengi ni majeruhi, adhabu za kadi zimekuwa zikifanya tusiwatumie wachezaji wengine kwa wakati," alisema kocha huyo.

Simba iliyoko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, imebakiza mechi dhidi ya Polisi Tanzania na Coastal Union, na zote zitachezwa Dar es Salaam.

Michezo
Ijumaa Juni 2, 2023
Nipashe



## Mourinho: Sifahamu hatima yangu Roma

UKURASA 21



Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said (katikati), akiwa na baadhi ya wanachama wa klabu hiyo 'ndani ya pipa' kuwafuata wapinzani wao, USM Alger kwa ajili ya mechi ya marudiano ya fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kesho nchini Algeria. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAFUNGUKA HAPATOSHI ALGERIA

## ●●●Majaliwa awataka Watanzania kuiombea Yanga ili ishinde kesho na...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akisema wachezaji wake wameahidi wanakwenda kupambana kwa kiwango cha juu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaomba Watanzania kuiombea Yanga ambayo inakwenda kucheza mechi ya marudiano ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji USM Alger itakayochezwa kesho nchini Algeria.

Msafara wa watu 259, wakiwamo wachezaji 29, benchi la ufundi, wafanyakazi, mashabiki na wadau mbalimbali wakiongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, waliondoka nchini jana kwa ndege maalum ya serikali iliyotolewa na Rais, Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza bungeni jijini, Dodoma jana, Waziri Mkuu, Majaliwa, alisema anaamini Yanga watashinda na kujenga historia ya Tanzania kupata kombe hilo kwa mara ya kwanza.

Wakati wa muda wa maswali ya papo kwa hapo kwa Waziri Mkuu, Majaliwa, alisema "Mnajua leo (jana) timu yetu ya Yanga ambayo inapeperusha bendera ya taifa itaondoka muda mfupi ujao kwenye uwanja wetu wa Dar es Salaam kuelekea Algeria kwa ajili ya mchezo wa pili.

Ninaamini sote na tuendelee kuiombea timu yetu Young African iweze kushinda mchezo huu wa pili kwa magoli mengi ya kutosha ili tuweze kuwa Tanzania mahiri. Timu yetu ina uwezo mkubwa, muhimu zaidi tuwaombee, mchezo wa tarehe tatu ninaamini Watanzania wote tutakuwa kwenye luninga kuiombea, na ninaamini tutashinda na kulileta kombe," alisema.

Majaliwa alisema anaungana na Rais Samia, ambaye ametoa usafiri wa ndege ambayo imebeba wachezaji, viongozi mbalimbali wakiwamo wa serikali na wapenzi wa soka ili kuisindikiza kwenye mashindano hayo muhimu kwa taifa.

"Tunatamani sana ushindi upatikane mkubwa ili tujenge historia ya kupata kombe hili kwa mara ya kwanza Tanzania. Mwenyezi Mungu awajalie safari njema na mchezo mwema na mafanikio makubwa kwenye mchezo wake," alisema Majaliwa.

Akizungumza muda mfupi kabla ya kuondoka, Nabi, alisema anafahamu zitakuwa ni dakika 90 ngumu, lakini wachezaji wake wamemhakikisha watapambana hadi 'tone' la mwisho la jasho na damu ili kupata ushindi.

"Muda ni mfupi, lakini nimewarudisha kwenye morali wachezaji wangu baada ya kupoteza mechi ya kwanza, walikuwa na presha kucheza mbele ya mashabiki, yote kwa yote mpira ndivyo ulivyo, tuna dakika 90 ngumu, lakini wachezaji wamenihakikishia watajitolea kupambana kwa dakika zote hadi mwisho wa mchezo, inawezekana tukabadilisha matokeo nchini Algeria," alisema Nabi.

Naye Chana alisema wanakwenda Algeria kupambana ili kupindua matokeo, huku akimshukuru Rais Samia kwa kutoa usafiri wa ndege kwenda katika fainali hiyo.

"Tumedhamiria, tumejipanga na tupo vizuri," alisema kwa kifupi waziri huyo.

Maneno yake hayakupishana na Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia, ambaye alisema msafara wote huo dhamira yao ni moja tu kuhakikisha wanapambana ili kombe lije Tanzania.

"Tunakwenda kupambana, wenzetu wameshinda hapa na sisi tunaweza kushinda kule, hii ni vita ya Watanzania wote, wala sio ya Yanga, lengo letu ni kupambana ili kombe lije Tanzania," alisema

INAENDELEA UK. 23

# Simba SC yajipanga kutorejea kinyonge

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' akisema maboresho makubwa yatakayofanyika katika kikosi hicho yataongeza ushindani ndani ya timu hiyo na kurejea kibabe baada ya kumaliza msimu huu kwa unyonge.

Simba imeshindwa kutwaa taji lolote msimu huu na katika mashindano ya kimataifa, kwa msimu wa tatu mfululizo ikitolewa kwenye hatua ya robo fainali.

Wekundu wa Msimbazi tayari wameanza mazungumzo na baadhi ya wachezaji ili kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao na mashindano ya kimataifa ya Super League watakayoshiriki.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji waowataka tayari majina yao yako mezani na uongozi uko katika hatua nzuri kwa ajili ya kuwanasa.

Ahmed alisema anaimani ujio wa nyota hao wapya utaongeza nguvu katika kikosi cha Simba na kurejesha furaha ambayo msimu huu imepotea.

Alisema wanatarajia kufanya mabadiliko makubwa kwa kuwaacha baadhi ya wachezaji kwa kufuata mapendekezo ya Robertinho na kusajili nyota wapya ambao ni wazoefu wa mashindano mbalimbali na wanatoka kwenye timu zilizofika hatua ya nusu au fainali ya Afrika.

"Majina ya wachezaji tunaowahitaji tayari yako mezani kwetu na kazi inaendelea kufanyika kikubwa tunafanya usajili kulingana na mahitaji ya timu kuleta wachezaji wenye uzoefu ambao wametoka kwenye klabu zao zimecheza michuano ya CAF kwa kuishia nusu au fainali" alisema Ahmed.

Aliongeza wanaendelea na usajili ili kukiandaa kikosi mapema kama mapendekezo ya kocha alivyotaka kuona wanasajili na kuingia kambini mapema kujiandaa na msimu mpya.

"Unajua Simba ni timu kubwa,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >